Jimbo la Illinois
Idara ya Huduma za Binadamu (DHS)



Programu ya Afua za Awali (EIP) Illinois

# Mwongozo kwa Familia

Januari 2026

IDHS
ILLINOIS DEPARTMENT OF HUMAN SERVICES

www.dhs.state.il.us
(800) 843-6154

**Shukrani**

Wafanyakazi wa Maktaba ya Afua za Awali (EIC) wanatoa shukrani kwa wajumbe wa Baraza la Ushauri kwa Wazazi (PAC), wafanyakazi wa CFC, IDHS na wadau wengine waliojitolea utaalamu, uzoefu, na maoni yao katika toleo hili la *Programu ya Afua za Awali Illinois: Mwongozo kwa Familia*. Tunatoa pia shukrani zetu za dhati kwa wafanyakazi wenzetu wa Ofisi ya Afua za Awali (BEI) katika Idara ya Huduma za Binadamu Illinois (IDHS) kwa kuunga kwao mkono toleo hili jipya.

Tunazitakia familia zote mafanikio mema katika safari yao ya miaka mitatu ya kwanza ya maisha ya mtoto wao mdogo. Tunatumaini kwamba mwongozo huu utatoa msaada wakati utakapokuwa katika Programu ya Afua za Awali Illinois.

*Ukiona picha hii, fahamu inatoka Maktaba ya EI (Clearinghouse) na ni rasilimali nzuri kwa familia za EI.*

Angalia Ninachoweza Kufanya

Tukianza Mapema Zaidi, Watafika Mbali Zaidi

The Illinois Early Intervention Program
**A Guide for Families**
July 2024, Swahili

Maktaba ya Afua za Awali Illinois (EIC)
Idara ya Elimu Maalum (DSE)
Chuo Kikuu cha Illinois Urbana-Champaign
Kituo cha Utafiti wa Watoto (CRC)
2202 Kirk Drive
Champaign, IL 61820-7469
(877) 275-3227
eiclearinghouse.org

# Yaliyomo

SEHEMU YA KWANZA

Karibu katika Programu ya Afua za Awali ya Illinois! ..... 1
- Hatua Muhimu za Ukuaji Kuanzia Kuzaliwa hadi Miaka 3 ..... 2
- Kwa Nini Huduma za Afua za Awali (EI) ni Muhimu? ..... 4
- Kisa cha Familia Moja katika Programu ya EI ..... 4
- Huduma za EI ni Zipi? ..... 5

SEHEMU YA PILI

Mtoto Wako Ana Ustahiki wa Programu ya EI? ..... 6
- Hatua ya 1: Wasiliana na Ofisi Yako Mahalia ya CFC ..... 6
- Hatua ya 2: Kutana na Mratibu wa Huduma ..... 6
- Hatua ya 3: Shiriki katika Upimaji na Tathmini ..... 6
- Hatua ya 4: Fahamu Kama Mtoto Wako Ana Ustahiki ..... 8
- Kubaini Ustahiki wa Huduma za EI ..... 9

SEHEMU YA TATU

Kushiriki katika Huduma za EI ..... 10
- Hatua ya 1: Andaa IFSP ..... 10
- Kujiandaa kwa IFSP ya Familia Yako ..... 12
- Hatua ya 2: Shiriki katika Huduma ..... 14
- Hatua ya 3: Amua Jinsi ya Kupokea Huduma ..... 17
- Hatua ya 4: Pitia IFSP Kila Baada ya Miezi Sita ..... 18
- Nini Kinafanyika Katika Ziara ya Kawaida ya EI? ..... 19

SEHEMU YA NNE

Kulipia Huduma za EI. ..... 20

SEHEMU YA TANO

Ni Wakati Gani wa Kuondoka Kwenye Programu ya EI? ..... 22

SEHEMU YA SITA

Haki Zako ni Zipi? ..... 24

SEHEMU YA SABA

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara na Familia ..... 27

NYONGEZA

Nyongeza A: Kanuni za Afua za Awali ..... 29
Nyongeza B: Faharasa ..... 30
Nyongeza C: Fasili za Huduma za EI ..... 35
Nyongeza D: Sampuli ya Maelezo/Barua pepe kwa Ofisi za CFC ..... 37
Nyongeza E: Rasilimali kwa Familia Zilizopo Katika Afua za Awali ..... 39
Nyongeza F: Matokeo: Kupima Mafanikio ya EI ..... 41
Nyongeza G: Maelezo ya Kikao Chetu cha IFSP ..... 42
Nyongeza H: Kanuni na Taratibu za Mazingira Halisi ..... 43
Nyongeza I: Sampuli ya Maelezo Kuhusu Maendeleo ya EI ..... 44

## Vipi Kama Nitahitaji Mkalimani?

Ukihitaji mkalimani, utapewa mmoja atayekusaidia katika mchakato mzima wa EI. Huduma hii inatolewa bure. Nyaraka za karatasi ngumu zinaweza pia kutafsiriwa katika lugha yako ya asili kama zitahitajika. Omba mkalimani wakati utakapowasiliana na ofisi yako ya CFC.

| | Jina | Simu |
|---|---|---|
| **CFC yangu Mahalia** | | |
| **Mratibu wa huduma** | | |
| **Msaidizi maalum wa wazazi (parent liaison)** | | |
| **Tarehe ya tathmini** | | |
| **Tarehe ya kikao cha IFSP** | | |
| **Watoa huduma** | | |
| **Rasimali muhimu za jumuiya** | | |
| **Wilaya mahalia ya shule** | | |



SEHEMU YA KWANZA

# Karibu katika Programu ya Afua za Awali ya Illinois!

Mwongozo huu ni kwa ajili yako, yaani mlezi mkuu wa mtoto wako. Una jukumu muhimu katika miaka ya awali ya mtoto wako kwa sababu unamjua mtoto wako vizuri, unasaidia ukuaji wa mtoto wako kila siku, na unajali kuhusu mustakabali wa mtoto wako.

Mwongozo huu, ambao mara nyingi huitwa "Mwongozo wa Familia", unaelezea programu ya Afua za Awali (EI), ikiwemo

- huduma zinazopatikana,
- ustahiki wa programu,
- haki zako, na
- jukumu lako la kupanga huduma kama mshiriki wa timu ya mwanao.



Pia kuna majibu ya maswali ambayo familia nyingi huuliza. Tunatumaini mwongozo huu utajibu maswali yako na kukusaidia kufanya maamuzi yatakayowapa wewe na mtoto wako mwanzo mzuri. Hapa Illinois, programu ya afua za awali inatolewa katika jumuiya yako mahalia kupitia ofisi za **Child and Family Connections (CFC)**. Mtu yeyote anaweza kumrufaa mtoto. Ushiriki ni hiari. Programu ya EI haihitaji uthibitisho wa hali ya uhamiaji.

Programu ya EI Illinois inatoa huduma mbalimbali kwa familia zenye watoto wadogo wenye **ulemavu** au **uchelewaji wa kukua**. Programu ya EI inajengwa na kanuni kwamba familia zote ziwasaidie watoto wao kujifunza na kukua. Familia zenye mtoto mwenye uchelewaji wa kukua au ulemavu zinaweza kuhitaji usaidizi ili kubaini njia bora za kumsaidia kukua. Familia zinashirikiana na wataalamu katika programu ya EI ili kumsaidia mtoto wao kuwa na mwanzo mzuri maishani. Mtu yeyote anaweza kumrufaa mtoto. Ushiriki ni hiari. Programu ya EI haihitaji uthibitisho wa hali ya uhamiaji. (Tazama Nyongeza A kwa Kanuni za Afua za Awali.)

Tathmini na huduma zote za EI ni siri. Hakuna taarifa kuhusu huduma za EI itakayoshirikishwa kwa watu wa nje ya familia yako na timu yako bila ridhaa yako.

## Nawezaje Kuipata Ofisi Mahalia ya CFC?

Programu ya EI inatolewa kupitia ofisi mahalia ya CFC. Kupata ofisi yako mahalia, piga (800) 843-6154 au tembelea Tovuti ya Kutafuta Ofisi za IDHS (IOL) kupitia www.dhs.state.il.us.

## Kwa Nini Baadhi ya Maneno Yamekozwa?

Maneno yaliyokozwa yapo katika Nyongeza B, faharasa inayoorodhesha na kufasili maneno mengi yanayotumiwa katika EI.

# Hatua Muhimu za Ukuaji Kuanzia Kuzaliwa hadi Miaka 3

Hatua muhimu zilizoorodheshwa hapa chini ni za kawaida kwa watoto. **Tafadhali kumbuka kwamba kila mtoto ni wa kipekee—na anakua na kupiga hatua kwa viwango vinavyotofautiana.** Mara nyingi tofauti hizi kati ya watoto wenye umri sawa si jambo la kuwa na wasiwasi nalo. Lakini kwa baadhi ya watoto, tofauti hizi zinaweza kuhusiana na uchelewaji wa kukua.

Hapa chini ni orodha ya hatua muhimu tangu kuzaliwa hadi miaka 3. Hata hivyo, tunakumbusha kwamba hatua muhimu zinaweza kuwa tofauti kwa watoto waliozaliwa kabla ya wakati (njiti). Kwa hatua muhimu za watoto njiti, tazama https://pathways.org/preemie-nicu/preemie/

**Katika miezi 2, watoto wengi wanaweza …**

- Kutulia wanapoongeleshwa au kubebwa
- Kutoa sauti nyingine tofauti na kulia
- Kukutazama wakati unapokuwa ukisonga
- Kuinua kichwa chao juu wakiwa wamelalia tumbo

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Hana mwitikio kukiwa na sauti kubwa
- Hatabasamu akisikia sauti yako
- Hafuati kwa macho vitu vinavyosonga

**Katika miezi 4, watoto wengi wanaweza …**

- Kutabasamu wao wenyewe ili kunasa umakini wako
- Kutoa sauti kama "oooo" na "aahh" (kicheko)
- Kuangalia mikono yao kwa kuvutiwa
- Kupeleka mikono yao mdomoni mwao

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Hapeleki mikono mdomoni mwake
- Hatafuti na kushika vichezeo
- Hakanyagi vizuri miguu yake ikiwa kwenye kiambaza kigumu

**Katika miezi 6, watoto wengi wanaweza …**

- Kuwatambua watu wanaowafahamu
- Kubadilishana kwa zamu kutoa sauti na wewe
- Kuweka vitu mdomoni mwao ili kuvichunguza
- Kujibiringiza akiwa amelalia tumbo ili alalie mgongo

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Misuli yake imekaza sana
- Amelegea sana
- Hana mwitikio kwa sauti
- Hajibiringizi (tumboni kwenda mgongoni)

**Katika miezi 9, watoto wengi wanaweza …**

- Kuonesha ishara kadhaa za uso (furaha, huzuni, hasira, mshangao)
- Kutoa sauti nyingi za aina mbalimbali, kama vile "mamamamama" na "bababababa"
- Kugonganisha vitu viwili kwa pamoja
- Kuketi wao wenyewe

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Haoneshi kuvutiwa na michezo ya kujificha uso au kupiga makofi
- Hatoi maneno ya kubwabwaja

**Katika miezi 12, watoto wengi wanaweza …**

- Kucheza nawe michezo kama kupiga makofi
- Kuelewa "hapana" (anasita kwa muda au kuacha unaposema hivyo)
- Kuweka kitu kwenye chombo, kama kichezeo ndani ya kikombe
- Kujinyanyua ili wasimame

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Hatafuti vitu vilivyofichwa
- Anapata tabu kujinyanyua ili kusimama
- Hamtafuti mtu mzima anayemfahamu anaposumbuliwa na kitu

**Katika miezi 15, watoto wengi wanaweza …**

- Kuiga watoto wengine wanapokuwa wakicheza (k.m., kutoa vichezeo kutoka kwenye chombo akiona mtoto mwingine amefanya hivyo)
- Kuangalia kitu walichokizoea unapokitaja
- Kujaribu kutumia vitu kwa njia sahihi, k.m., simu, kikombe, au kitabu
- Kupiga hatua kadhaa wao wenyewe

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Haonekani kujua matumizi ya vitu vya kawaida vya nyumbani (k.m., brashi, simu, uma, kijiko)
- Hafanyi juhudi ya kupiga hatua yeye mwenyewe

**Katika miaka 18, watoto wengi wanaweza …**

- Kusogea mbali na wewe lakini wakihakikisha upo karibu nao
- Kujaribu kutamka maneno matatu au zaidi tofauti na "mama" au "dada"
- Kukuiga wakati ukifanya shughuli za nyumbani (kufagia kwa ufagio)
- Kutembea bila kumshikilia yeyote au chochote

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Hawezi kutembea
- Haongei angalau maneno 15
- Anamuepuka mzazi anapokuwa akisumbuliwa na kitu

**Katika miaka 2, watoto wengi wanaweza …**

- Kugundua pale wengine wanapokuwa wameumia au kuudhika
- Kupiga mpira
- Kuonesha vitu katika kitabu anapoulizwa, kama "Mbuzi yuko wapi?"
- Kuonesha angalau sehemu mbili za mwili anapoulizwa
- Kucheza na zaidi ya kichezeo kimoja kwa wakati, kama vile kuweka chakula cha kuchezea kwenye sahani ya kuchezea
- Kutamka angalau maneno mawili kwa pamoja "mama moo"

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Hatumii sentensi za maneno mawili
- Haigi vitendo au maneno
- Hafuatishi maelekezo rahisi ya hatua moja

**Katika miezi 30, watoto wengi wanaweza …**

- Kucheza kando ya watoto wengine na wakati mwingine kucheza nao
- Kutamka takribani maneno 50
- Kufuata maelekezo ya hatua mbili "Weka hiyo chini na funga mlango"
- Kuruka juu kwa miguu yote miwili

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Hatamki neno lolote
- Hafuatishi maelekezo ya hatua moja

**Katika miaka 3, watoto wengi wanaweza …**

- Kuwatambua watoto wengine na kujiunga nao katika mchezo
- Kutamka jina lao la kwanza, akiulizwa
- Kuchora duara ukimuonesha jinsi ya kufanya hivyo
- Kutumia kijiko

Unaweza kuwa na wasiwasi ikiwa mtoto wako …

- Ana matamshi yasiyoeleweka
- Hawezi kusaidia kuvaa na kuvua nguo yeye mwenyewe
- Anapata tabu kutumia ngazi na kusimama thabiti

Chanzo: Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDCP)

https://www.cdc.gov/act-early/resources/milestone-checklists.html

## Kwa Nini Huduma za Afua za Awali (EI) ni Muhimu?

Kuna sababu kadhaa kwa nini huduma za EI ni muhimu:

- Katika miaka mitatu ya kwanza, ubongo na mwili wa mtoto wako hukua kwa haraka sana. Mtoto wako ataongezeka ukubwa zaidi ya mara mbili kila mwaka. Uchelewaji wa kukua mara nyingi unagundulika baada ya mtoto kutofikisha hatua muhimu za ukuaji. Unaweza kukagua ukuaji wa mtoto wako dhidi ya orodha ya hatua muhimu zilizoorodheshwa katika kurasa zilizopita.
- Ikiwa mtoto wako alizaliwa kabla ya wakati au alikuwa mdogo sana, anaweza kuhitaji usaidizi ili kukua kama watoto wengine wa umri wake.
- Ikiwa mtoto wako alizaliwa na ulemavu, anaweza kuhitaji msaada zaidi ili kujifunza na kukuza stadi mpya.
- Ikiwa mtoto wako anakua taratibu sana au tofauti, basi EI inaweza kuwasaidia wewe na mtoto wako kuendelea kujifunza na kukua.
- Ikiwa mtoto wako yupo katika hatari ya uchelewaji wa kukua, EI inaweza kusaidia kuboresha stadi na utendaji wa mtoto wako.

Programu ya EI inaweza pia kuisadia familia yako na wengine kujua uwezo na mahitaji ya mtoto wako. Kumbuka, miaka mitatu ya kwanza ya mtoto wako ni msingi wa maisha. Kama mlezi wa kwanza kabisa wa mtoto wako, una jukumu muhimu katika ukuaji wa mtoto wako. Afua za awali zinatambua umuhimu wa uhusiano kati ya mzazi na mtoto. Kuna njia kadhaa ambazo afua za awali zitamnufaisha mtoto wako, wewe na familia yako:

- Utajifunza mbinu mpya za kushugulikia mahitaji ya mtoto wako. Timu yako ya afua za awali itakupa mafunzo ya mbinu ambazo zitamsaidia mtoto wako kupiga hatua.
- Utahisi kuwa umewezeshwa kumtetea mtoto wako.
- Utakuwa na uelewa mkubwa kuhusu haki zako na huduma ambazo mtoto wako anapewa.

### Kisa cha Familia Moja Katika Programu ya EI

Nilikuwa najiuliza iwapo mtoto wangu anakua sawa sawa. Carson alikuwa na miezi 8 na bado hakuwa amejaribu kujibiringiza. Alikuwa akilala kwa tabu na alikuwa akisumbua wakati wote. Alionekana kuwa mgumu kuliko watoto wengine niliowajua. Hivyo, nikaongea na daktari wetu wa watoto, na akatupa rufaa kwenda Ofisi ya Child and Family Connections. Wanaijua kazi yao vizuri! Walielewa wasiwasi wangu na kunisikiliza. Walinitazama nikicheza na Carson na wakapendekeza kwamba afanyiwe tathmini na timu ya wataalamu. Nilikuwepo wakati wa tathmini na nilishirikisha taarifa na rekodi zake za kitiba.

Baadaye, tulikutana na wakaniambia Carson alikuwa na dalili za uchelewaji wa kukua katika miendo na maendeleo ya kijamii na kihisia. Tuliandaa mpango wa huduma, na mratibu wangu wa huduma alinisaidia kuchagua tabibu wa maungo (PT) na tabibu wa ukuaji (DT). Nilifarijika kujua kwamba nilikuwa sahihi kuomba msaada. Tulipewa huduma za PT kwa takribani mwaka mmoja, na zilikuwa na mchango mkubwa katika kumsaidia Carson kuwa mchunguzi zaidi, kujibiringiza, kisha kutambaa, na hatimaye kutembea na kukimbia. Pia nilijifunza jinsi ya kumpa hamasa na kuunga mkono juhudi zake na kumsukuma ajaribu zaidi. Tabibu wa ukuaji alishirikiana nasi hadi Carson alipofikia umri wa miaka 3. Alinisaidia kuandaa ratiba na alinionesha njia mbalimbali za kucheza na kujenga mahusiano na mwanangu. Nilijihisi kama sehemu ya timu. Jambo hili lilibadili kabisa maisha ya familia yetu.

## Huduma za EI ni Zipi?

Huduma za EI zimebuniwa kukidhi mahitaji ya mtoto wako katika maeneo haya ya ukuaji::

- Kimwili (jinsi mtoto wako anavyosonga na kuchunguza)
- Kiakili (jinsi mtoto wako anavyojifunza)
- Kuwasiliana (jinsi mtoto wako anavyokufahamisha kile anachohitaji)
- Kijamii na kihisia (jinsi mtoto wako anavyohusiana nawe na kuonesha hisia zake)
- Kubadilika kulingana na mazingira (jinsi mtoto wako anavyoshiriki shughuli za kila siku za kujijali)



Huduma za EI zinaweza kujumuisha:

- Huduma za kisaikolojia/ushauri nasaha
- Huduma za kitiba (kwa madhumuni ya uchunguzi na upimaji tu)
- Lishe
- Lugha ya ishara au lugha ya mikono
- Macho
- Mafunzo na usaidizi kwa familia
- Matibabu ya audiolojia/usikiaji
- Teknolojia saidizi (AT)
- Tiba Maungo (PT)
- Tiba Vitendo (OT)
- Tiba ya Matamshi-Lugha
- Tiba ya ukuaji/mafunzo maalum
- Ukalimani na utafsiri katika lugha nyingine
- Uratibu wa huduma
- Usafiri
- Ushauri wa kiafya
- Ustawi wa jamii
- Uuguzi

Tazama Nyongeza C kwa fasili na mifano ya kila moja ya huduma hizi. Ikiwa mtoto wako atakuwa na ustahiki wa programu ya EI, huduma zitaamuliwa katika kikao cha IFSP. Huduma pendekezwa zinatokana na kiasi cha usaidizi unaohitajika kuisaidia familia yako kufikia matokeo/malengo mliyoandaa wakati wa kikao cha IFSP. Utoaji wa huduma hizi unapaswa kuendana na mapendeleo ya mtoto na familia yako, mtindo wa ujifunzaji, na imani za kitamaduni.

SEHEMU YA PILI

# Mtoto Wako Ana Ustahiki wa Programu ya EI?

Hizi hapa ni hatua za kujua iwapo mtoto wako ana ustahiki.

### Nini Kinampa Mtoto Wangu Ustahiki wa Huduma?

Mtoto wako mdogo (mchanga hadi miezi 36) ana ustahiki wa huduma kupitia programu ya EI Illinois ikiwa ...

- ana uchelewaji wa 30% katika angalau eneo au nyanja moja ya ukuaji,
- ana ugonjwa unaojulikana kusababisha tatizo la uchelewaji wa kukua au ulemavu, au
- yupo katika hatari kubwa ya uchelewaji mkubwa wa kukua.

## Hatua ya 1: Wasiliana na Ofisi Yako Mahalia ya CFC

Unaweza kuwapigia Ofisi yako mahalia ya Child and Family Connections (CFC) ili kuongea na mratibu wa huduma kuhusu wasiwasi wako. Ukihitaji usaidizi wa kupata ofisi yako mahalia ya CFC, tafadhali tembelea Tovuti ya Kutafuta Ofisi za IDHS kupitia www.dhs.state.il.us (chini kabisa ya ukurasa mkuu) au piga (800) 843-6154. Daktari wako au mlezi anaweza pia kukupa rufaa kwenda ofisi mahalia. Mara baada ya kuwasiliana na CFC, watachagua mratibu wa huduma ili kukutana na familia yako na kuzungumza nawe kuhusu jinsi ambavyo programu ya EI inaweza kusaidia ukuaji wa mtoto wako.



## Hatua ya 2: Kutana na Mratibu wa Huduma

Katika kikao chenu cha kwanza mratibu wa huduma atakuelezea programu ya EI na kusaidia kuweka mipango ya upimaji na tathmini. Hii inaitwa **kikao cha awali (intake meeting)** kwa sababu utaombwa kushirikisha taarifa kuhusu mtoto wako na familia yako. Mratibu wa huduma atakuuliza maswali kuhusu ukuaji na maendeleo ya mtoto wako, historia ya kitiba, na shughuli zako za kila siku (muda wa kucheza, milo, ratiba ya kulala, ulezi wa mtoto, n.k.). Unaweza pia kupewa orodha maalum ya kubaini stadi na uwezo wa mtoto wako.

Utaombwa kusaini fomu za ridhaa na kukubali kwamba mratibu wa huduma anaweza kushirikisha taarifa kuhusu mtoto wako kwa timu ambayo itampima na kumtathmini mtoto wako na inayoweza kukusaidia kupanga huduma za EI. Ukiridhia, basi mtoto wako anaweza kupewa rufaa ya kufanyiwa upimaji na tathmini. Mchakato huu ni bure kwa familia zote.

## Hatua ya 3: Shiriki katika Upimaji na Tathmini

Wewe ndiye unayemjua mtoto wako vizuri zaidi; unajua mtoto wako anachokipenda na asichokipenda. Uelewa wako huu unakufanya kuwa

mshirika muhimu kwenye timu ya mtoto wako. Timu itajumuisha wewe, mratibu wa huduma, na angalau watoa huduma wengine wawili wa EI. Idadi ya wajumbe wa timu inaweza kutofautiana kulingana na mahitaji ya mtoto wako na inaweza kujumuisha wataalamu mbalimbali, kama vile tabibu wa ukuaji na tabibu maungo. Timu itampima na kumtathmini mtoto wako katika **maeneo** yote matano ya ukuaji:

- Kimwili (jinsi mtoto wako anavyosonga na kuchunguza),
- Kiakili (jinsi mtoto wako anavyojifunza),
- Kuwasiliana (jinsi mtoto wako anavyokufahamisha kile anachohitaji),
- Kijamii na kihisia (jinsi mtoto wako anavyohusiana nawe na kuonesha hisia zake), na
- Kubadilika kulingana na mazingira (jinsi mtoto wakoanavyoshiriki shughuli za kila siku za kujijali).



Wajumbe wa timu watamchunguza na watahusiana na mtoto wako. Wanaweza kupima uwezo wa mtoto wako na kuulinganisha dhidi ya hatua muhimu za ukuaji (tazama ukurasa wa 2). Wanaweza kumchunguza na kumhusisha mtoto wako katika shughuli ili kuona anachoweza kufanya na anachopenda kufanya. Watakuuliza maswali kama vile:

- Je, mtoto wako anakua kwa namna unayotegemea akue?
- Je, una wasiwasi kuhusu ukuaji wa mtoto wako?
- Je, mtoto wako anafanya mambo tofauti na ndugu zake au watoto wengine unaowajua katika umri huu?
- Je, ratiba za familia yako zipoje, kama vile muda wa kuoga na kula?
- Je, mtoto wako ana mwitikio gani wakati wa shughuli za familia?
- Je, vipi ni **vipaumbele** vya familia yako kwa mtoto wenu?
- Je, unahitaji nini ili kuisaidia familia yako kuwa makini na vipaumbele hivyo?

**“Mchakato wa afua za awali ulikuwa mpya kabisa kwetu na kwa kiasi fulani ulituogopesha. Mratibu wetu wa awali wa CFC alikuwa vizuri sana. Alitumia muda kuelezea hatua zote katika mchakato, daima alisisitiza kwamba uamuzi wowote ulikuwa ni wetu tu, na alihakikisha kwamba tulikuwa na utambuzi wa chaguzi zote zinazopatikana kwetu. Nilihisi kwamba alimjali mwanetu kweli kweli.”**

**“**

**Kulea mtoto wangu aliyezaliwa kabla ya wakati (njiti) ilikuwa furaha na changamoto kwa wakati mmoja. Timu yangu ya afua za awali ilinisaidia kupata zaidi ‘furaha’ katika suala la uzazi kwa kunionesha njia mbalimbali za kumsaidia mtoto wangu kusonga na kucheza na kula na kulala. Imani yangu iliongezeka sana, huku mtoto wangu akiongezeka mita na kilo kadhaa kwa sababu ya usaidizi wao!**

**”**

Ikiwa lugha yako ya asili si Kiingereza, programu ya EI itakupa mkalimani, kama atapatikana, kwa ajili ya upimaji na tathmini. Hutatozwa gharama yoyote kwa huduma ya mkalimani. Nyaraka za karatasi ngumu zinaweza pia kutafsiriwa katika lugha ya asili ya familia yako kama zitahitajika.

## Hatua ya 4: Fahamu Kama Mtoto Wako Ana Ustahiki

Mtoto wako atakuwa na ustahiki ikiwa ana ulemavu ambao unaweza kuchelewesha ukuaji wake au ikiwa tathmini itaonesha mtoto wako ana uchelewaji wa kukua wa 30% au juu zaidi katika nyanja moja au zaidi. Mtoto wako anaweza kuwa na ustahiki wa afua za awali ikiwa yupo katika mfumo wa ustawi wa watoto wa jimbo. Mtoto wako pia anaweza kuwa na ustahiki ikiwa yupo katika hatari ya uchelewaji wa kukua kwa sababu ana vihatarishi vitatu au zaidi, kama vile mlezi mkuu anatumia kupita kiasi pombe au vilevi vingine, mama mzazi alitumia kupita kiasi pombe au vilevi vingine wakati wa ujauzito, mlezi wake mkuu ana miaka chini ya 15, familia haina makazi, mlezi wake mkuu ana ugonjwa sugu, au mlezi wake mkuu ana elimu ya gredi la 10 au chini ya hapo. Kwa orodha kamili ya vihatarishi, tazama https://www.dhs.state.il.us/page.aspx?item=96963


Ustahiki wa afua za awali haumaanishi moja kwa moja kwamba mtoto wako amethibitishwa rasmi kitiba kuwa na tatizo au ulemavu. Inaweza kumaanisha tu kwamba mtoto wako ana uchelewaji unaoweza kutibiwa na huduma zitolewazo na programu ya afua za awali. Baada ya tathmini kukamilika, utaarifiwa na CFC kama mtoto wako ana ustahiki. Una haki ya kupata ripoti za tathmini. Ikiwa mtoto wako ana ustahiki na ukaamua kwamba unataka kushiriki katika programu ya EI, basi kikao kitafanyika kati yako na timu yako ili kuandaa **Mpango Binafsi wa Huduma kwa Familia (IFSP)**. Uandaaji wa mpango ni bure na kikao cha IFSP lazima kifanyike ndani ya siku 45 baada ya mtoto wako kupewa rufaa kwenda programu ya EI.

Ingawa si lazima, unaweza kuomba matokeo ya tathmini kabla ya kikao. Hii inaweza kukusaidia kujiandaa kwa ajili ya kikao kwa kuisoma ripoti, kuandaa maswali ya kuiuliza timu, na kutoa maoni ya ziada. Tazama Nyongeza D kwa sampuli ya barua ya kuomba matokeo ya tathmini kabla ya kikao.

Ikiwa mtoto wako hatakuwa na ustahiki, basi IFSP haitaandaliwa na hakuna huduma za EI zitakazotolewa. Mratibu wa huduma anaweza kukupa orodha ya rasilimali za jumuiya zinazoweza kukidhi mahitaji ya familia na ya mtoto wako. Ukiwa na wasiwasi mpya kuhusu ukuaji wa mtoto wako, unaweza kuwasiliana na ofisi ya CFC wakati wowote kabla ya mtoto wako kufikisha miaka 3 ili kujadili wasiwasi wako. Tunatoa orodha ya rasilimali muhimu katika Nyongeza E.

## Kubaini Ustahiki wa Huduma za EI

**Tarehe**



SEHEMU YA TATU

# Kushiriki katika Huduma za EI



Familia zinazochagua kushiriki katika programu ya EI zinashirikishwa katika maamuzi yote kuhusu huduma za EI. Wewe ni mjumbe wa timu ya mtoto wako. Hatua ya kwanza ni Mpango Binafsi wa Huduma kwa Familia (IFSP). Baada ya wewe na timu kukamilisha mpango, utausaini ili kuonesha unakubaliana na huduma. Huduma lazima zianze ndani ya siku 30 baada ya kusaini IFSP. Mpango utaelezea huduma gani zitatolewa, mara ngapi, na zitatolewa na nani. Kwa sababu watoto wachanga na wadogo wanajifunza vizuri zaidi kupitia uzoefu na miingiliano ya kila siku, huduma zitatolewa nyumbani kwako au katika mazingira mengine ya kawaida. Kwa sababu ya ratiba za kazi au mahitaji mengine, baadhi ya familia huhitaji watoa huduma waje mahali mtoto wao hutumia muda mwingi. Hii inaweza kuwa kituo cha kulea watoto au nyumba ya rafiki au ndugu. Wewe na timu yako mtafanya mapitio ya mpango na maendeleo ya mtoto wako angalau kila baada ya miezi sita. Unaweza kukubali, kukataa, au kusitisha huduma wakati wowote. Ushiriki wako ni hiari na unahitaji ridhaa yako ya maandishi. Sehemu ifuatayo inaelezea mchakato wa utoaji wa huduma kwako na kwa mtoto wako.

## Mratibu Wako wa Huduma za EI . . .

- ndiye mhusika wako wa kwanza katika mfumo wa EI
- anaitambulisha familia yako kwa wafanyakazi wa CFC, akiwemo msaidizi maalum wa wazazi.
- anaratibu ufanyaji tathmini na kubaini ustahiki wa huduma,
- anazisaidia familia kuelewa majukumu na haki zao katika mfumo wa EI,
- anaisaidia familia na wajumbe wengine wa timu ya EI kuandaa na kutekeleza IFSP,
- anawasiliana na familia kila mwezi wakati mtoto anapokuwa katika EI,
- anaandaa na kutunza rekodi za suala husika (huduma) la mtoto na la familia, na
- anaisaidia familia kuondoka katika huduma za EI kipindi mtoto akifikisha miaka 3.

## Hatua ya 1: Andaa IFSP

Mratibu wako wa huduma na timu yako ya IFSP watakusaidia

- kutambua wasiwasi na vipaumbele vya kukidhi mahitaji ya mtoto wako,
- kuandaa **matokeo** ya IFSP kwa ajili ya mtoto wako na familia yako,
- kukubali huduma na usaidizi ili kumsaidia mtoto wako na familia yako kukidhi matokeo hayo yaliyotambuliwa, na
- kuamua iwapo huduma zinalipiwa ada..

Mnapaswa kufanya kikao cha kuandaa IFSP mapema iwezekanavyo ila isizidi siku 45 tangu mtoto wako kupewa rufaa kwenda programu ya EI. Hakuna tozo wala gharama za kuandaa mpango. Mratibu wako wa huduma na timu yako ya EI watakusaidia.

### *IFSP ni Nini?*

IFSP ni mpango ambao unauandaa pamoja na timu yako ya EI. Mpango huu unaakisi vipaumbele na wasiwasi wako kwa mtoto wako. Wewe ndiye unayebaini matokeo (k.m., mtoto wako kutembea, mtoto wako kutamka neno, mtoto wako kuwa wa kwanza kukumbatia) ambayo unayataka kwa mtoto na familia au walezi wako. Hizi ni kauli ambazo zinaelezea mabadiliko na faida ambazo unataka kuziona kwa mtoto wako na familia yako. Wewe na timu yako pia mtabaini huduma za kufikia matokeo haya.

Unaweza kuanza kwa kuuliza maswali mawili: Faida gani nataka mtoto na familia yangu izipate kutoka EI? Nini kitakuwa tofauti au bora kwa mtoto wangu na familia yangu wakati mabadiliko haya yatakapofanyika?

Huduma zilizoainishwa katika IFSP zinakusudia kuunga mkono matokeo makuu matatu:

- Kupata na kutumia maarifa na ujuzi.
- Kujenga mahusiano chanya ya kijamii.
- Kutumia tabia sahihi kukidhi mahitaji yake.

Itajumuisha pia **matokeo ya familia**. Matokeo matatu muhimu (tazama Nyongeza F) yanajumuisha

- kuelewa nguvu, uwezo na mahitaji ya mtoto wako;
- kumsaidia mtoto wako kukua na kujifunza; na
- kujua haki zako za kisheria kuhusiana na huduma za mtoto wako.

### *Nani Anapaswa Kuhusishwa katika Kuandaa IFSP?*

Mratibu wako wa huduma atakuelezea mchakato wa IFSP na kupanga kikao cha kuweka mipango ya IFSP. Mratibu wa huduma atashirikiana nawe kupanga tarehe na eneo ambalo linafaa kwako. Utapata notisi ya maandishi inayothibitisha kikao husika. Kikao kinapaswa kuendeshwa kwa lugha yako ya asili. Unaweza kuomba mkalimani ikiwa unazungumza lugha tofauti na Kiingereza na utapewa mmoja, ikiwa atapatikana.

Kikao kitajumuisha wewe, mratibu wa huduma, na timu ya kufanya tathmini. Unaweza kualika familia, marafiki, au mtu yeyote atakayehusika.

Ili kusaidia kujiandaa na kikao cha IFSP, unaweza kujaza katarasi-kazi ya "Kujiandaa kwa IFSP ya Familia Yako" kwenye ukurasa wa 12 na 13 wa mwongozo huu. Kumbuka kwamba wewe ni mshirika mwenye haki sawa katika kupanga na kuunda mpango huu. Tunathamini mawazo na ushiriki wa familia yako. Unaweza kutumia Nyongeza G ili kukusaidia kuhifadhi maelezo muhimu kuhusu vikao hivi.

### *Kwa Nini IFSP Inatakiwa Kusainiwa?*

Mara baada ya wewe na timu yako kukubaliana matokeo na huduma za IFSP, utasaini na kupewa nakala ya mpango. Saini yako inaonesha umeukubali mpango kama ulivyoandikwa, au mabadiliko uliyoainisha katika ukurasa wa utekelezaji. Mratibu wako wa huduma pia atakusaidia kubaini iwapo utahitajika kulipa ada ya kila mwezi ya ushiriki wa familia katika huduma za EI kulingana na kipato cha familia yako na mambo mengine. (Kwa maelezo zaidi, tazama Sehemu ya 4, "Kulipia Huduma za EI.")

## Msaidizi Wako Maalum wa Wazazi . . .

- pia alikuwa na mtoto aliyepokea huduma za afua za awali,
- anatoa shughuli zilizo rafiki kwa mtoto,
- anaziunganisha familia na familia nyingine,
- anazitaarifu familia kuhusu hafla za jumuiya na vikundi vya kucheza,
- anazielimisha familia kuhusu haki zao,
- anajibu maswali,
- anashirikisha rasilimali, na
- anazifundisha familia kuwa watetezi.

# Kujiandaa kwa IFSP ya Familia Yako

**1. Kuna mambo ambayo nataka kila mtu ayajue kuhusu mtoto wangu na familia yangu:**

**2. Wasiwasi mpya ambao umeibuka tangu kikao cha mwisho tulichofanya na mratibu wangu wa huduma:**

**3. Hivi ndivyo mtoto wangu anavyowasiliana na mimi na wengine:**

**4. Hizi ni njia ambazo mtoto wangu anapenda kujifunza mambo mapya:**

**5. Hivi ndivyo mtoto wangu anavyofanya wakati anahitaji msaada:**

**6. Hizi ni stadi na tabia ambazo ningependa kuona mwanagu akizifanya katika miezi 6-12 ijayo:**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**7. Hasa, ningependa kuona mtoto wangu akionesha stadi na tabia hizi mpya wakati wa ratiba au shughuli hizi:**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**8. Haya ni mambo ambayo ningependa kujifunza katika miezi 6-12 ijayo:** ______________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**9. Njia ambazo familia yangu na mimi tunajifunza vizuri zaidi:** ______________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## Hatua ya 2: Shiriki katika Huduma

### *Nani Anatoa Huduma za EI?*

Mratibu wako wa huduma atakupa chaguo la watoa huduma za EI waliopo kutoa huduma za EI zilizoainishwa katika IFSP. Chaguo lako la watoa huduma linaweza kuwa na kikomo kwa sababu ya upatikanaji, bima, au mahitaji mengine ya kipekee ya mtoto wako. Chaguzi zako pia zinaweza kuwa na kikomo kulingana na jinsi unavyotaka kupokea huduma. Unaweza pia kuomba kubadilishiwa mtoa huduma na/au mratibu wa huduma wakati wowote, na kwa sababu yoyote. Tunatoa sampuli ya barua ya kubadili watoa huduma na nyingine ya kuomba mratibu mpya wa huduma katika Nyongeza D.



### *Vipi Kama Nikitaka Kubadilisha Huduma?*

Unaweza kumwomba mratibu wako wa huduma kupanga kikao pamoja na timu yako ya IFSP ili kujadili mabadiliko katika IFSP yako, kama vile kuongeza, kupunguza, kuzidisha huduma kwa mtoto wako. Tazama Nyongeza D, sampuli ya barua ya kuomba kubadili huduma.

### *Huduma za EI Zinatolewa Wapi?*

Huduma za EI zinapaswa kutolewa katika **mazingira halisi** ya mtoto. Hii inamaanisha mahali ambapo mtoto wako anatumia muda wake mwingi na ambapo watoto wengine wadogo wasio na ulemavu au tatizo la uchelewaji wa kukua wanapotumia muda wao mwingi. Mazingira halisi yanaweza kuwa nyumbani kwako, kituo cha ulezi wa watoto, maktaba, nyumbani kwa ndugu, au mahali kwingine ambapo kwa kawaida familia yako inatumia muda mwingi. Mazingira halisi hukuwezesha wewe na mtoa huduma ya EI kutumia ratiba zenu za kila siku kumfundisha mtoto wako stadi au tabia mpya. Shughuli hizi zikiweza kujumuishwa katika ratiba ya kila siku ya mtoto wako, wewe na walezi wengine mtaweza kuzifanya mara kwa mara zaidi na mtoto wako wakati mtoa huduma ya EI asipokuwepo. Kanuni muhimu zinazohusiana na mazingira halisi zimewekwa katika Nyongeza H.

Ni muhimu kukumbuka kwamba, bila kujali mahali huduma za EI zinapotolewa, modeli ya kufundisha inatumika katika afua za awali. Hii

inamaanisha wakati za ziara za EI mtoa huduma anaweza kukusaidia wewe (au mlezi) kuingiliana na mtoto wako ili kusaidia ukuaji wake. Kufundisha inaweza kukusaidia kubaini mbinu za kumsaidia mtoto wako, kufanyia kazi mbinu hizo wakati wa ziara, kutafakari miingiliano yako na mtoto wako, kutatua changamoto, na kupata mrejesho kutoka kwa mtoa huduma za EI.

### *Nini cha Kutegemea Wakati wa Ziara ya EI?*

Wewe na mtoa huduma za EI mnapaswa kukubaliana muda na tarehe ya kukutana. Katika kikao cha kwanza, kuna uwezekano mkubwa mtoa huduma za EI akajadili ukuaji wa sasa wa mtoto wako na kupitia maswali na wasiwasi wa familia yako. Atapendekeza njia unazoweza kuzitumia kwa mtoto wako ili kufikia matokeo ya IFSP. Mtoa huduma za EI atakuchukulia wewe au mlezi mkuu wa mtoto wako kama mshirika katika utoaji wa huduma za EI. Hii inamaanisha kwamba utaombwa kushiriki kivitendo wakati wa ziara za EI. Mtoa huduma za EI hapaswi kuwa peke yake na mtoto wako.



### *Unawezaje Kushiriki katika EI?*

Kushirikiana na mtoa huduma za EI ni muhimu sana, ili uweze kusaidia ujifunzaji na ukuaji wa mtoto wako. Mtoa huduma za EI atakusanya taarifa kwa kuzungumza nawe na wanafamilia au walezi wengine. Mtoa huduma za EI atajifunza uwezo wa mtoto wako na mahitaji yake kwa kukuchunguza wewe na mtoto wako katika shughuli za kawaida. Tumia karatasi-kazi ya “Kujiandaa kwa IFSP ya Familia Yako” kuongoza mazungumzo yako na watoa huduma za EI.

Uzoefu chanya, na saidizi wa watu wazima anaowajua husaidia ubongo wa mtoto wako kuwa thabiti na kubadilika-badilika. Hii inakufanya wewe kuwa mtu unayeweza kuleta matokeo makubwa sana kwenye ukuaji wa mtoto wako. Kama mjumbe muhimu wa timu ya EI ya mtoto wako, unaweza kusaidia kwa kufanya yafuatayo:

- Wafahamu watoa huduma wako wa EI.
- Shiriki kivitendo katika ziara za mtoto wako.
- Waombe watoa huduma wako wa EI wafafanue shughuli wanazozifanya na wewe na mtoto wako na sababu ya kutumia ya shughuli hizo.
- Shirikisha taarifa kuhusu ratiba zako, desturi na tamaduni za familia.
- Ongelea sehemu mbalimbali ambazo wewe na mtoto mnazitembelea, kama vile viwanja vya michezo na nyumbani kwa marafiki.
- Waelezee watu ambao wewe na mtoto wako mnafurahia kuwa nao.
- Zingatia kile ambacho mtoto wako anavutiwa nacho.
- Mwambie mtoa huduma wasiwasi wowote ulionao kuhusu mtoto wako.

- Jifunze shughuli za kuendeleza ukuaji wa mtoto wako na zijumuishe kwenye ratiba zako na za mtoto wako za kila siku.
- Toa fursa nyingi kwa mtoto wako kucheza na kufanyia kazi stadi mpya katika ratiba za kila siku, kama vile kuvaa, muda wa chakula, na kubadilisha nepi.
- Tambua usaidizi na rasilimali rasmi na zisizo rasmi za familia yako. Kwa mfano, nani uwasiliane naye kwa msaada? Nini ulichonacho tayari ambacho unaweza kukitumia kutoa usaidizi kwako na kwa mtoto wako?



- Omba msaada ukihitajika. Wafahamishe familia, marafiki, na watoa huduma za EI jinsi ambavyo wanaweza kutoa msaada wakati wa nyakati ngumu.
- Cheza na ongea na mtoto wako mara kwa mara. Hii itamfanya ajue yeye ni wa kipekee na anapendwa!

**Ni muhimu kuhakikisha mpango wako unafanya kazi. Ongea mara kwa mara na msaidizi wa wazazi au mratibu wa huduma.**

### *Wewe na Mtoa Huduma za EI Mtawasiliana Vipi Kuhusu Ziara za EI?*

Watoto wanaweza kupokea huduma za EI katika maeneo mengi, ikiwemo kituo cha ulezi, nyumba ya familia, na maeneo ya jumuiya. Usipoweza kuwepo wakati wa ziara ya EI, mtoa huduma za EI anapaswa kukupa taarifa muhimu kuhusu ziara husika. Kwa mfano, ikiwa mtoto wako anapokea tiba ya matamshi na lugha katika kituo chake cha ulezi, mwombe mtoa huduma za EI na mtoa huduma za ulezi wakujulishe kuhusu ziara. Wanaweza kukutumia barua pepe yenye muhtsari wa ziara. (Tazama Nyongeza I kwa sampuli ya ripoti ya maendeleo.) Wanaweza pia kurekodi video ya kipande cha ziara ya EI kwa ridhaa yako ili uweze kuona nini mtoto wako anajifunza na jinsi unavyoweza kusaidia kuendeleza ujifunzaji wa mtoto wako. Unaweza pia kuomba kupigiwa simu ili kujadili ziara na mikakati ya jinsi unavyoweza kumsaidia mtoto wako. Unapaswa kupewa taarifa mara kwa mara kutoka kwa watoa huduma za EI ikiwa hutakuwepo wakati wa ziara za EI.

### *Unawezaje Kukutana na Wazazi Wengine wa Programu ya EI?*

Ofisi yako mahalia ya CFC ina **msaidizi maalum wa wazazi** mwenye uzoefu wa mfumo wa huduma za EI kwa sababu yeye ni mzazi au mlezi wa mtoto mwenye tatizo la uchelewaji wa kukua au ulemavu. Jukumu la msaidizi huyu ni kutoa taarifa na usaidizi kwa familia. Unaweza kumwomba

- akupe taarifa kuhusu uchunguzi wa kitiba wa mtoto wako,
- akusaidie kumtetea mtoto wako,
- atoe usaidizi binafsi ambao unaweza kuuhitaji wakati fulani, na
- akuunganishe na wazazi wengine.

Pia Maktaba ya Afua za Awali ya Illinois (http://eiclearinghouse.org) ni chanzo kizuri cha taarifa za bure kwa ajili yako. Ukiwa na maswali unaweza kutembelea tovuti, kupata taarifa katika maktaba yao, kupewa majarida, na kupiga simu au kutuma barua pepe. Mtaalamu wa EI atawasiliana nawe ndani ya saa 48 ili kukujibu maswali au maombi yako.

## Hatua ya 3: Amua Jinsi ya Kupokea Huduma

Wewe na timu yako mtajadili jinsi huduma za EI zitakavyotolewa. Chaguzi zinajumuisha.

**Ziara za Ana kwa Ana:** Huduma za EI zinatolewa kwa ushirikiano kati ya mzazi au mlezi na mtoa huduma za EI, wakiwepo kimwili katika eneo moja, iwe ni nyumbani au mazingira ya jumuiya. Hii ni njia ya kawaida ya kutoa huduma za EI.



**Ziara za video mbashara:** Huduma za EI zinatolewa kupitia Intaneti kwenye kompyuta au tableti (k.m., iPad), jambo linaloiwezesha familia yako kushirikiana na mtoa huduma katika wakati halisi.

**Mashauriano kupitia simu:** Huduma za EI zinatolewa na mtoa huduma za EI katika wakati halisi kwa njia ya simu lakini bila video. Hii ni njia ya muda mfupi tu ya kupokea huduma.

**Mseto:** Huduma za EI zinatolewa kwa mchanganyiko wa ziara za ana kwa ana, ziara za video mbashara, na mashauriano kupitia simu. Hii huzipa familia uwezo wa kuitikia wasiwasi wa kiafya wa mtoto/kaya na vipaumbele vingine vya familia vinavyoweza kusababisha ziara za EI kusitishwa.

Haijalishi namna gani unapokea huduma,

- zitajenga juu ya uwezo wa mtoto na familia yako na kukidhi mahitaji ya mtoto na familia yako kwa njia zinazozingatia na kuthibitisha utamaduni na lugha ya familia yako;
- zitajengwa juu ya matokeo yako yaliyobainishwa katika IFSP;
- Zitatumia mbinu ya kufundisha ili kutoa huduma na kuweka mkazo kwenye kujenga uwezo wa mlezi;
- zitaweka mkazo kwenye fursa za kujifunza na afua zitakazojumuishwa kwenye ratiba na shughuli za kawaida za familia yako;
- hazitahitaji au kutarajia watoto kuketi na kuhudhuria kwa vipindi virefu vya muda;

- zitazingatia mahitaji na mapendeleo ya ratiba zako;
- zitazingatia faragha, kanuni za usiri, na masuala ya ulinzi wa kisheria; na
- zitafanywa kuwa binafsi kwako na rahisi ili kuendana na vipaumbele na mazingira yako kadri yanavyobadilika.

Uamuzi wa jinsi ya kupokea huduma unafanywa na wajumbe wote wa timu ya IFSP na kutegemea na mambo mengi, kama upatikanaji wa watoa huduma za EI katika eneo lako, ufikio na ufahamu wako wa teknolojia, na uvumilivu wako wa suala la kukaribiana na watoa huduma za EI nyumbani kwako au mazingira mengine unayoyajua. Zungumza na mratibu wa huduma na timu yako ya EI kuhusu chaguo lipi ni bora kwako. Daima unaweza kubadili mawazo yako kuhusu unavyopokea huduma.

## Hatua ya 4: Pitia IFSP Kila Baada ya Miezi Sita

IFSP inaweza kubadilishwa. Kadri mtoto wako anavyokua na kupiga hatua, mambo muhimu kwako yanaweza kubadilika, na hivyo kuhitaji huduma mpya au tofauti. Timu ya EI inaweza kubadilisha huduma ili kukidhi vizuri zaidi mahitaji ya mtoto na familia yako.

Wewe na timu yako ya IFSP mtapitia maendeleo ya mtoto kila baada ya miezi sita na kuboresha mpango angalau mara moja kwa mwaka. Mahitaji yako yakibadilika, wewe na timu yako mnaweza kukutana mara nyingi zaidi ili kuubadili mpango kadri itakavyohitajika.

Ili kujiandaa na mapitio ya IFSP, unaweza kujiuliza maswali haya yafuatayo:

- Je, mtoto amepiga hatua?
- Je, matokeo ya sasa yanahitaji huduma tofauti au za ziada?
- Je, vipaumbele vya mtoto wako vimebadilika?
- Je, huduma gani mtoto wako anaweza kuzihitaji siku za usoni?
- Je, mtoto wako amefikisha matokeo ya IFSP? Je, matokeo mapya yanafaa?
- Je, familia yako imefikisha matokeo ya IFSP? Je, matokeo mapya yanahitajika?

Dhumuni la mapitio ya IFSP ni kubaini iwapo mtoto wako anaendelea kuwa na ustahiki wa programu ya EI au iwapo mtoto wako amefikisha hatua muhimu za ukuaji na hivyo kutohitaji tena huduma.

## Nini Kinafanyika Katika Ziara ya Kawaida ya EI?

EI inaweka mkazo kwa mtoto na familia, hivyo katika ziara ya kawaida ya EI mtoa huduma huifundisha familia mbinu za kutumia kwa mtoto. Kwa lengo lengo hili, ziara ya kawaida ya huduma za EI huwa inajumuisha mengi ya matendo yafuatayo:

- **Kupanga mapema ziara.** Mtoa huduma anapitia maelezo na shughuli na mikakati ya mpango kwa ajili ya ziara. Mzazi au mlezi anaweza naye pia kupitia maelezo ya kikao kilichopita. Ikiwa ni ziara ya video mbashara, mtoa huduma anaweza kukutumia (au mlezi) baadhi ya vichezeo na vitu ya kuandaa kwa ajili ya ziara.

- **Kuwasili na kusalimiana.** Mtoa huduma atawasili na kuzungumza na mzazi au mlezi; watabaini malengo ya ziara na kujiandaa kuanza.

- **Kushiriki shughuli zinazoweka mkazo kwenye matokeo.** Mtoa huduma na mzazi au mlezi wanashirikiana na mtoto mchanga/mdogo.

- **Kuchunguzana.** Mzazi au mlezi anaweza kumchunguza mtoa huduma akiingiliana na mtoto wake, na mtoa huduma naye pia atamchunguza mzazi au mlezi na mtoto wakiingiliana na kutoa mrejesho stahiki.

- **Kuonesha na kufanyia kazi shughuli na mbinu mipya.** Mtoa huduma anaweza kumuonesha mzazi au mlezi njia mpya au tofauti za kumsaidia mtoto wake kujifunza.

- **Kushirikishana taarifa na maarifa.** Mtoa huduma na mzazi au mlezi, wote wawili, wanaweza kuwa na taarifa muhimu za kushirikishana kuhusu ukuaji, huduma, usaidizi, na maendeleo ya mtoto.

- **Kuandika kumbukumbu ya huduma zilizotolewa.** Mtoa huduma ataacha taarifa ya maandishi kwa ajili ya mzazi au mlezi kuhusu kilichotokea wakati wa ziara. Hii ni muhimu hasa wakati ambapo huduma zinatolewa wakati mwanafamilia hayupo, kama vile katika kituo cha ulezi wa watoto.

- **Kupanga shughuli na mbinu kati ya ziara moja na nyingine.** Mtoa huduma anaweza kumsaidia mzazi au mlezi kufikiria jinsi ya kujumuisha shughuli walizojifunza kwenye ratiba zao za kila siku. Wanaweza pia kubaini taarifa ambazo mtoa huduma au mlezi anaweza kuzikusanya kwa ajili ya ziara ijayo ya EI.

- **Kupanga ratiba ya ziara ijayo.** Ili kuhakikisha kwamba huduma zinaendelea bila kukatizwa, mzazi au mlezi na mtoa huduma za EI wanapanga ratiba ya ziara ijayo ya EI.

SEHEMU YA NNE

# Kulipia Huduma za EI

Familia zenye watoto wenye ustahiki wa Programu ya Afua za Awali (IEP) Illinois mara nyingi huwa na maswali kuhusu kulipia huduma.

## Huduma Zipi za EI NI Bure?

Tathmini zote na uratibu wa huduma unaotolewa kupitia programu ya EI ni bure. Mtoto wako akiwa na ustahiki na mkaingia katika programu ya EI, wafanyakazi watashirikiana nawe kuandaa na kuratibu Mpango wako Binafsi wa Huduma kwa Familia (IFSP) bila gharama yoyote. Ikiwa unazungumza lugha tofauti na Kiingereza, programu ya EI itatoa huduma ya mkalimani na utafsiri wa lugha bila malipo.



## Ada ya Ushiriki wa Familia ni Nini?

Unaweza kulazimika kulipa ada ya kila mwezi ya ushiriki wa familia ambayo itategemea na kipato chako, ukubwa wa familia, na iwapo una gharama nyingi za matibabu/maafa za kulipia mwenyewe. Mratibu wako wa huduma anaweza kukupa taarifa kwamba ada yako itakuwa kiasi gani. Ikiwa hutaki kufichua kipato chako, basi utalipia ada ya juu kabisa. Taarifa za kila mwezi zitatumwa kwa familia yako zikionesha malipo ya kila mwezi pamoja na kiasi ambacho mfumo umekilipia kwa ajili ya huduma za mtoto wako. Familia kamwe hazipaswi kulipia ada zaidi kuliko mfumo kwa ajili ya huduma. Kwa maelezo zaidi, tafuta ada “family participation fee" kwenye tovuti ya IDHS kupitia https://www.dhs.state.il.us.

## Vipi Kama Nikitumia Bima Yangu Binafsi?

Bima binafsi ya afya inaweza kusaidia kupunguza kiasi ambacho programu ya EI inalipia huduma kwa ajili ya mtoto wako. Bima binafsi ya afya ikitumika kwa ajili ya huduma, malipo ya EI pia yanaweza kukusaidia kukidhi makato yako ya mwaka ya bima ya afya. Pia, kamwe hutatozwa au kutegemewa kulipia malipo shirikishi kwa ajili ya huduma za EI. Huduma zozote zinazokingwa na bima binafsi ya afya zinatozwa kwa programu ya EI. Unapaswa kujadili na mratibu wako wa huduma kuhusu bima yako binafsi ya afya na mchakato wa kutoza bili.

## Kutoa Ufikio wa Mafao Yangu ya Umma, Kama Vile All Kids, Kunaisaidiaje Programu ya EI?

Programu ya EI inaweza kulipwa fidia kwa huduma fulani ikiwa familia zitatoa ufikio huu. Hii inatoa uwezekano wa chanzo kingine cha mapato kwa programu nzima ya EI. Ikiwa huna mafao ya umma ila unadhani unaweza kuwa na ustahiki, ongea na mratibu wa huduma kuhusu kutuma maombi ya All Kids. Familia zisizo na bima zinahimizwa sana kujaza maombi ya All Kids na kutembelea tovuti ya Get Covered Illinois kupitia https://getcovered.illinois.gov/

## "Kutoa Ridhaa" Ya Kutumia Bima Inamaanisha Nini?

Utaombwa kusaini fomu ya ridhaa ambayo inaiwezesha programu ya EI Illinois kuwasiliana na kumtoza bili mtoa bima yako au All Kids kwa huduma za EI ambazo familia yako inazipokea.



## Kwa Nini Programu ya EI Illinois Isilipe Tu Kila Kitu?

Programu ya EI ni "mlipaji wa mwisho." Hii inamaanisha fedha nyingine zote zilizopo lazima zitumike kwanza. Programu ya EI inapokea fedha kutoka seriakli kuu, lakini fedha hizi haziwezi kukidhi gharama nzima ya programu. Serikali ya Jimbo pia inatoa pesa za kusaidia programu ya EI. Pesa kutoka bima binafsi na ada za ushiriki wa familia ni msaada muhimu kwa programu. Zinaisaidia programu kuendelea kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa familia zote zenye ustahiki.

## Kwa Maelezo Zaidi

Ukiwa na maswali zaidi, tafadhali wasiliana na mratibu wako wa huduma katika ofisi yako mahalia ya CFC. Unaweza pia kupata taarifa muhimu kutokaOfisi Kuu ya Kutoza Bili ya EI (CBO) kupitia https://eicbo.info.

SEHEMU YA TANO


# Ni Wakati Gani wa Kuondoka Kwenye Programu ya EI?

Mtoto wako anaweza kuondoka kwenye programu ya EI baada ya ukuaji wake kuimarika na matokeo ya mtoto wako kuwa yamefikiwa. Vinginevyo, mtoto wako anaweza kubaki katika programu ya EI hadi afikishe miaka mitatu, au **huduma za ziada** zikiwa chaguo kwa mtoto. Angalau miezi sita kabla ya mtoto wako kufikisha miaka 3, wewe au timu yako ya IFSP mtaanza kupanga kuondoka kwenye huduma za EI. Hii itakupa muda wa kufahamu iwapo mtoto wako ana ustahiki wa huduma za elimu maalum ya utotoni (ECSE) kupitia wilaya mahalia ya shule au, kulingana na tarehe yake ya kuzaliwa, iwapo mtoto wako ana ustahiki wa huduma za ziada. Si watoto wote watakuwa na ustahiki wa ECSE, na mtoto wako anaweza kuhitaji kufanyiwa tathmini nyingine.

Kimsingi, ukiomba teknolojia saidizi lakini kuna chini ya miezi sita kabla ya mtoto wako kufikisha umri wa kuondoka kwenye afua za awali, mtoto wako anaweza kutopokea teknolojia saidizi kutoka afua za awali. Katika Nyongeza E, tumeorodhesha rasilimali zinazoweza kumsaidia mtoto wako kupata **teknolojia saidizi** katika kipindi hicho.

*Kitabu hiki kinaziongoza familia za Illinois katika kipindi cha mtoto wao kuondoka kwenye EI na kuingia ECSE.*

*Kinapatikana tu kwa Kingereza na Kispaniola*




https://www.isbe.net/Documents/When-Im-Three.pdf

## Huduma za Mpito

Hizi ni hatua husika na jukumu lako katika mchakatos:

**Hatua ya 1:** Zungumza na mratibu wako wa huduma, msaidizi maalum wa wazazi, na watoa huduma za EI kuhusu namna ya kumwandaa mtoto na familia yako kwa ajili ya mpito.

**Hatua 2:** Mratibu wako wa huduma atakuuliza iwapo unataka kupewa rufaa kwenda wilaya mahalia ya shule kwa ajili ya huduma za ECSE. Unaweza kukubali au kukataa. Ukikubali, saini yako inahitajika ili kushirikisha taarifa kwa wilaya yako mahalia ya shule.

**Hatua 3:** Hudhuria mkutano wa kupanga kipindi cha mpito cha mtoto wako.

**Hatua 4:** Ikihitajika, shiriki katika tathmini za wilaya ya shule za mtoto wako.

**Hatua ya 5:** Pata uamuzi kuhusu ustahiki wa mtoto wako katika ECSE, huduma za ziada za EI, marekebisho, na huduma kutoka wilaya ya shule.

**Hatua ya 6:** Akiwa na ustahiki, weka mipango ya Mpango Binafsi wa Elimu (IEP) au mpango wa Section 504. Kama hana, fikiria rasilimali nyingine za jumuiya kwa mtoto wako.

## Huduma za Ziada

Familia zenye ustahiki zinaweza kuendelea kupokea huduma za EI hata baada ya mtoto wao kufikisha miaka mitatu hadi kuanza kwa mwaka unaofuta wa masomo baada ya *vigezo vyote vifuatavyo* kufikiwa. Mtoto lazima

- awe na IFSP iliyo hai,
- siku yake ya kuzaliwa iwe kati ya Mei 1 na Agosti 31, na
- ana ustahiki wa Programu ya Elimu Binafsi (IEP) katika wilaya mahalia ya shule ya mtoto.

Ili kufahamu zaidi kuhusu ustahiki wa huduma za ECSE, tembelea ISBE kupitia https://www.isbe.net/ na utafute "early childhood special education services."

## Kutathmini Huduma Zako za EI

Muda mfupi baada ya kuondoka katika programu ya EI, utapewa utafiti wa matokeo ya familia kutoka programu ya Mafunzo ya EI Illinois. Huu ni utafiti *muhimu sana*, na tunaomba ujibu maswali yake na kuyarejesha mapema iwezekanavyo. Majibu yako yatasaidia programu ya EI kupata taarifa muhimu kuhusu uzoefu wa familia yako katika programu ya EI na ikiwezekana kufikiria mabadiliko kama yatahitajika. Utafiti unauliza kuhusu **matokeo ya familia** kama vile

- kuelewa nguvu, uwezo na mahitaji ya mtoto wako;
- kumsaidia mtoto wako kukua na kujifunza; na
- kujua haki zako.

Unauliza pia kuhusu manufaa ya mfumo wa EI. Utafiti huu unaweza kujibiwa kwa njia mbalimbali na unapatikana kwa Kiingereza na Kispaniola. Kuwa huru kuwasiliana na Programu ya Mafunzo ya EI ya Illinois (nambari zimewekwa kwenye utafiti) ukihitaji msaada kujibu utafiti.



SEHEMU YA SITA

# Haki Zako ni Zipi?



Programu ya EI ya Illinois ilianzishwa na sheria ya jimbo ili kupatana na Sehemu C ya **Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu** (IDEA) ya serikali kuu. IDEA inajumuisha huduma za EI kwa watoto wenye ustahiki kuanzia kuzaliwa hadi wanapofikisha miaka mitatu au ikiwezekana hadi kuanza kwa mwaka unaofuata wa masomo baada ya kufikisha miaka mitatu. Baada ya kufikisha miaka 3, IDEA itaainisha kuwa mtoto wako anaweza kuendelea kupokea huduma kutoka wilaya yako mahalia ya shule. IDEA inaelezea haki zako kama mzazi wa mtoto anayepokea huduma za EI.

Baadhi ya haki za uzazi zimeelezewa hapa kwa ufupi. Kwa taarifa zaidi kuhusu haki za familia katika EI, tembelea eiclearinghouse.org na utafute “family rights.” Taarifa zaidi za kina zinapatikana hapa:

- Kijitabu cha “Infant/Toddler & Family Rights Under IDEA for the EI system” kupitia https://www.childfind-idea-il.us/Materials/4392.pdf
- Vituo vya Taarifa za Mafunzo kwa Wazazi (PTICs) Illinois: Kimsingi wafanyakazi wa vituo vya PTIC ni wazazi wa watoto wenye matatizo ya ulemavu au uchelewaji wa kukua. Vituo vya PTIC vinatoa mafunzo ya bure, taarifa, na huduma za kutoa rufaa kwa familia zenye watoto wanaopokea huduma za afua za awali, shule na huduma za watu wazima. Taarifa zaidi, tazama https://eiclearinghouse.org/blogs/parent-centers/
- Mwongozo kwa wazazi wa “Educational Rights and Responsibilities: Understanding Special Education in Illinois” unapatikana kupitia https://www.childfind-idea-il.us/Materials/Educ_Rights_en.pdf

Hapa Illinois, kuna vituo viwili vya PTIC:

- Family Resource Center on Disabilities (FRCD) Kituo kinahudumia jiji la Chicago. Tembelea http://frcd.org, wapigie FRCD kupitia (312) 939-3513, au watumie barua pepe info@frcd.org.
- Family Matters kinahudumia jimbo lote. Tembelea http://fmptic.org au piga (866) 4FMPTIC.

## Ridhaa Baada ya Kuarifiwa

**Ridhaa** inamaanisha kwamba unatoa ruhusa ya wewe na mtoto wako kupokea huduma. Unaombwa kusaini waraka wa IFSP ili kuonesha kwamba unaelewa na kuukubali mpango husika na huduma zilizobainishwa ndani yake. Pia utaombwa kusaini ridhaa za kushirikisha taarifa kuhusu mtoto na familia yako kwa watoa huduma za afua za awali au mashirika mengine ambayo yanamhudumia mtoto na familia yako. Taarifa inaweza kushirikishwa tu ikiwa umesaini fomu inayoonesha nani atapokea taarifa hiyo. Taarifa zote zinapaswa kutolewa kwa lugha ya kawaida unayoitumia.

## Notisi Iliyoandikwa Kabla

Notisi ya maandishi lazima itolewe kwako kabla ya shirika la EI au mtoa huduma za EI kufanya badiliko katika huduma za EI za mtoto wako. Notisi lazima itolewe kwa lugha ya kawaida unayoitumia. Unapaswa kupokea notisi ya maandishi kuhusu kikao chochote, ili uwe na muda wa kutosha wa kufanya taratibu za kuhudhuria.

## Mapitio ya Rekodi

Una haki ya kupitia rekodi zozote zinazohusiana na huduma za EI za mtoto wako. Rekodi zinapaswa kupatikana kwako ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kuziomba. Unaweza kuomba kurekebisha rekodi. Shirika likikataa kurekebisha rekodi, una haki ya kuomba usikilizaji wa shauri la utaratibu wa haki.

## Usiri wa Rekodi

Rekodi zote za huduma za EI za familia yako ni siri. Watoa huduma wako watashirikishana taarifa wao kwa wao ili kutoa huduma bora kwa familia yako. Rekodi zitashirikishwa tu kwa wengine kama inavyoruhusiwa na sheria za faragha k.m., Sheria ya Uhamishaji na Uwajibikaji wa Bima ya Afya (HIPAA) na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA). Wewe na familia yako mnapojiandaa kuondoka programu ya EI, utaombwa kutoa ridhaa ya maandishi kabla rekodi zako kutolewa kwa wilaya eneo la shule au shirika lingine ambalo litamhudumia mtoto wako akifikisha miaka 3.

## Utatuzi wa Wasiwasi

Ukiwa na wasiwasi wowote kuhusu huduma, au usipokubaliana na maamuzi kuhusu mtoto wako, unapaswa kuzijadili na mratibu wako wa huduma katika CFC. Huduma hizi au maamuzi haya yanaweza kuhusiana na mambo kama utambuzi, upimaji, ufanyaji tathmini, uchaguliwaji, au

usahihi wa huduma. Usiporidhika na matokeo ya majadiliano, chaguzi rasmi za usuluhisho wa kiutawala zimeainishwa katika sheria. Hizi zinajumuisha:

**1. Malalamiko kwa jimbo.** Unaweza kufungua lalamiko la maandishi, lililosainiwa, katika Idara ya Huduma za Binadamu Illinois (IDHS) ukidhani mtoa huduma amekiuka sheria au kanuni kuhusu Sehemu C ya Programu ya Afua za Awali. Maelezo lazima yajumuishe vielelezo vinavyothibitisha lalamiko lako. IDHS inaweza kutumia Programu ya Kufuatilia Afua za Awali Illinois (EIMP) kufanya uchunguzi (https://earlyinterventionmonitoring.org).

IDHS ina siku 60 tangu kupokea lalamiko kuchunguza na kuandika uamuzi wake. Katika kipindi hiki, IDHS inaweza kufanya uchunguzi wa kujitegemea. Uamuzi wa IDHS lazima ujumuishe gunduzi kutokana na uchunguzi, matokeo, na sababu za kutoa uamuzi wa mwisho. Ikiwa lalamiko litagundulika kuwa la kweli au halali, basi uamuzi lazima ujumuishe taratibu za kusahihisha chanzo cha lalamiko.

**2. Upatanishi.** Ikiwa kuna hali ya kutokukubaliana kati yako na mtoa huduma mahalia, CFC, au IDHS, unaweza kuomba **upatanishi**. Upatanishi ni kikao cha hiari kinachosimamiwa na mpatanishi mwenye sifa katika eneo rahisi kwako ndani ya siku 10 baada ya kutoa ombi. Jukumu la mpatanishi ni kusaidia wahusika wasiokubaliana kuzungumza na kufikia mwafaka. Mpatanishi hawezi kulazimisha makubaliano. Majadiliano yanayofanyika wakati wa upatanishi ni siri. Upatanishi ni hiari, na unapaswa kukubali kwa uhuru kushiriki. Serikali ya jimbo inalipia gharama za upatanishi. Makubaliano ya upatanishi yanarekodi masharti yaliyokubaliwa. Huduma zilizokubaliwa hapo awali kwa mtoto wako zinapaswa kuendelea wakati wa kipindi cha upatanishi.

**3. Usikilizaji wa shauri la utaratibu wa haki.** Unaweza kuomba usikilizaji wa shauri la taratibu za haki (due process hearing) ili kutatua lalamiko kwa mtoa huduma wako au CFC. Ukiomba usikilizaji wa shauri la taratibu za haki, wewe na CFC yako mna hadi siku 30 za kutatua lalamiko hadi uridhike. Usiporidhika, usikilizaji wa shauri la taratibu za haki utafanyika.

Usikilizaji wa shauri la taratibu za haki ni sawa na kesi ya mahakamani. Usikilizaji huu lazima ufanyike kwa muda na mahali ambapo ni rahisi kwako. Afisa wa usikilizaji wa shauri atasikiliza pande zote za kutokubaliana. Afisa wa usikilizaji wa shauri hapaswi kuwa mwajiriwa wa shirika lolote au chombo kingine kinachotoa huduma za EI kwa mtoto wako. Wakati wa usikilizaji wa shauri, unaweza kuja na **mwanasheria, wakili**, au rafiki mwenye uelewa au mafunzo maalum kuhusu mtoto wako au kuhusu watoto wenye ulemavu. Una haki pia ya kuja na mtoto wako na kuruhusu usikilizaji wa shauri uwe wazi kwa umma. Ili kupata wakili, unaweza kuwasiliana na Equip for Equality, shirika la Mfumo wa Ulindaji na Utetezi Illinois https://equipforequality.org/.

Una haki ya kupewa nakala ya rekodi za usikilizaji wa shauri, gunduzi, na maamuzi, bila gharama yoyote. Uamuzi kwa maandishi unapaswa kutumwa kwako ndani ya siku 45 baada ya kipindi cha usuluhisho cha siku 30 kumalizika. Upande ulioshindwa una haki ya kukata rufani dhidi ya uamuzi.

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara na Familia

## Nimuulize Nini Msaidizi Wangu Maalum wa Wazazi wa CFC?

- Zipi ni baadhi ya rasilimali bora katika jumuiya kwa ajili yangu na familia yangu?
- Kuna viwanja vya michezo vya jumuiya ambavyo mtoto wangu anaweza kuvitumia?
- Unaweza kuniunganisha na wazazi wengine?

## Nini Maana ya Maneno Yote Yanayotumika Katika EI? Wapi Nitapata Taarifa Zaidi Kuhusu Ulemavu wa Mwanangu?

Kama ilivyo kwa programu nyingi za huduma, programu ya EI ina maneno mengi ya kuelezea programu, huduma, na watoa huduma. Faharasa katika Nyongeza B itakusaidia kuelewa maneno hayo. Unaweza pia kutembelea Maktaba ya Afua za Awali ya Illinois (EIC) kupitia http://eiclearinghouse.org/. Maktaba ya EI Illinois imeandaliwa kwa ajili ya familia zinazotumia huduma na zinazotaka kufahamu zaidi. Inatoa orodha kuu ya huduma kwa jimbo la Illinois na inatumika kama rasilimali inayotoa taarifa mbalimbali za EI. Kwa kutumia kiungo katika katalogi ya maktaba kwenye tovuti yake, unaweza kuazima vitabu na video (bure) zitakazokusaidia wakati wa uwepo wako katika programu ya EI na kuendelea!



## Vipi Kama Familia Yangu Itahama Nje ya Kanda Yangu ya CFC au katika Jimbo Tofauti?

Mjulishe mratibu wako wa huduma ikiwa unahama au huna tena anwani ya kudumu. Ikiwa unahamia ndani ya Illinois, mratibu wako wa huduma atakusaidia kuhamia kwenye CFC mpya kwa kuwasilisha nakala ya rekodi za mtoto wako kwenye ofisi ya CFC inayohudumia jumuiya yako mpya. Ofisi

mpya ya CFC itawasiliana nawe ili kupanga huduma za EI katika eneo lako jipya mapema iwekanavyo ikiwa watoa huduma wako wa mwanzo wa EI hawapatikani tena. Ikiwa unahamia jimbo tofauti, mratibu wako wa huduma anaweza kusaidia kukuunganisha kwenye programu ya EI katika jimbo lako jipya.

## EI Inatoa Huduma za Kitiba?

Hapana. Programu ya EI inatoa huduma za ukuaji ili kumsaidia mtoto wako kukua na kujifunza. Huduma za kitiba zinaweza tu kutolewa kwa madhumuni ya uchunguzi wa kitiba na tathmini na si kwa matibabu.



## Naweza Kubadili Mtoa Huduma wa EI au Mratibu wa Huduma?

Ndio. Kunaweza kuwa na nyakati ambapo baadhi ya familia zinajikuta ratiba zao haziendani na ratiba ya mtoa huduma ya EI na zingependa kuwa na mtoa huduma anayeweza kukutana katika muda unaofaa zaidi. Au familia inaweza kupendelea mtizamo tofauti. Kama watoa huduma ya EI wengine watakuwepo, basi badiliko linaweza kufanyika baada ya kuombwa. Ikiwa kuna hali ya kutokubaliana katika huduma zako za EI, unapaswa kuzungumza na mratibu wako wa huduma. Ikiwa bado una wasiwasi, basi unaweza kupitia haki zako kama zilizovyoelezwa katika kijitabu cha “Infant/Toddler & Family Rights Under IDEA” na kufikiria chaguzi za kutatua wasiwasi wako.

Ikiwa utahitaji mratibu mpya wa huduma kwa sababu yoyote ile, tafadhali kumbuka CFC inaweza kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya kupangiwa kazi nyingine haraka. Hili likitokea, unapaswa kujadili na meneja wa CFC kuhusu kipindi cha muda wa kubadili waratibu wa huduma. Tazama Nyongeza D kwa sampuli ya barua ya kuomba mratibu mpya wa huduma.

NYONGEZA A

# Kanuni za Afua za Awali

*Imekubaliwa na Baraza la Mashirika Mbalimbali ya Illinois kuhusu Afua za Awali (IICEI)*

Imeandaliwa Oktoba 2001
Mara ya mwisho kupitiwa Januari 2021

1. Lengo kuu la afua za awali (EI) ni kuwajengea uwezo walezi kwa kusaidia uwezo wao wa kuendeleza ukuaji bora wa mtoto wao na kuwezesha ushiriki wa mtoto wao kwenye familia na shughuli za jumuiya.

2. Shabaha ya EI ni kuwezesha ushiriki wa kivitendo wa familia katika mchakato wa EI kwa kuwashirikisha walezi katika upangaji na utekelezaji wa huduma, ikiwemo kuingiza mbinu ya afua kwenye maisha ya familia, kama vile ratiba, shughuli, na miingiliano pamoja na mtoto wao. Familia/walezi ndiyo wanaotoa EI halisi kwa kutumia kibunifu mbinu zao za ulezi ili kuwezesha ukuaji wa mtoto wao, huku wakiweka usawaziko katika mahitaji ya watu wengine katika familia.

3. EI inahitaji uhusiano wa ushirikiano kati ya familia na wataalamu, huku kukiwa na ushiriki sawa kwa wale wote wanaohusika katika mchakato. Ushirikiano na mazungumzo endelevu na yanayozingatia usawa kati ya familia na wataalamu yanahitajika ili kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, na kurekebisha mikakati na huduma za afua.

4. Afua zinapaswa kuunganishwa na matokeo mahsusi, yanayoweka mkazo kwa familia, yanayofanya kazi, na yanayopimika ya Mpango Binafsi wa Huduma kwa Familia (IFSP) ambayo yamebuniwa kwa kutumia taratibu zinazothibitisha na kuzingatia tamaduni na lugha.

5. Huduma na afua zitajumuishwa kwenye IFSP iliyochanganuliwa kwa kina ambayo itazihitaji familia na wataalamu kushirikiana ili kubadilishana mara kwa mara maarifa na taarifa wao kwa wao. Pia inahitaji kushirikiana katika taaluma mbalimbali ndani ya mfumo mpana wa utotoni ili kuongeza uwezo wa timu kutatua kwa pamoja matatizo na kutekeleza afua. Mpango utajengwa juu ya uwezo, vipaumbele, rasilimali, ratiba, na shughuli za familia na kuepuka kurudiwa huduma kusiko lazima. Huduma na mikakati inatokana na utafiti bora uliopo, taratibu zinazopendekezwa katika medani, na sheria na kanuni za elimu maalum.

6. Huduma, afua, na maendeleo yanapaswa kufuatiliwa mara kwa mara kupitia uchunguzi na mijadala endelevu na wajumbe wote wa timu ili kuhakikisha kwamba mbinu zilizotekelezwa zina mafanikio katika kufikia matokeo.

7. Mawasiliano na ushirikiano endelevu pamoja na wataalamu wa EI, wanafamilia, na wataalamu katika mifumo ya ubia nje ya EI, ambao wanaisaidia kila familia, yanahimizwa. Mawasiliano endelevu na jumuishi kati ya wajumbe wote wa timu huwezesha huduma zilizoratibiwa, zinazozingatia tamaduni, na za kina katika mifumo yote ili kufikia vizuri zaidi vipaumbele vya familia, mazingira yanayobadilika, na vipindi vya mpito.

8. Watoto na familia zao katika programu ya EI wanastahili kuwa na huduma zenye ubora wa hali ya juu kadri iwezekanavyo. Viwango vya hali ya juu vitawekwa kwa ajili ya kutoa mafunzo na kuidhinisha wafanyakazi wa utawala na afua. Mafunzo, usimamizi, na teknolojia zitatumika kwa lengo la kuongeza umahiri.

NYONGEZA B

# Faharasa

**Afua za Awali**
*Early Intervention*
Huduma maalum zinazotolewa kwa watoto wadogo wanaoonesha ishara au walio katika hatari ya *uchelewaji wa kukua* (tazama hapo juu) Huduma zinapangwa na kutekelezwa pamoja na familia na mara nyingi pamoja na timu yenye wataalamu mbalimbali. (tazama pia *Programu ya Afua za Awali Illinois*.)

**Akili**
*Cognitive*
Eneo la ukuaji ambalo linahusisha stadi za kufikiria, ikiwemo ujifunzaji na stadi za kutatua matatizo.

**Bodi ya Elimu ya Jimbo la Illinois**
*Illinois State Board of Education*
Shirika la jimbo ambalo linasimamia huduma za elimu kwa watoto wenye miaka 3 hadi 21 katika jimbo la Illinois.

**Elimu Maalum ya Utotoni**
*Early Childhood Special Education*
Huduma za ECSE kwa watoto wenye miaka 3-5 wenye tatizo la uchelewaji wa kukua au ulemavu na familia zao zinatolewa kupitia wilaya mahalia za shule na vyama vya elimu maalum katika mazingira ya darasa la elimu ya awali.

**Huduma za Ziada za Afua za Awali**
*Early Intervention Extended Services*
Huduma za ziada zinaziwezesha familia zenye ustahiki kuendelea kupokea huduma za EI baada ya mtoto wao kufikisha miaka mitatu hadi mwanzoni mwa mwaka unaofuata wa masomo, wakati watakapoanza kupokea elimu maalum ya utotoni kupitia wilaya yao mahalia ya shule.

**Idara ya Huduma za Binadamu Illinois**
*Illinois Department of Human Services*
Shirika la jimbo ambalo limechaguliwa kama shirika kuu kwa ajili ya programu ya EI Illinois.

**IDEA**
Tafadhali tazama *Sheria ya Elimu kwa watu wenye Ulemavu (IDEA) au Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (Sehemu C).*

**Idhini ya Afua za Awali**
*Early Intervention Credential*
Idhini inatolewa kulingana na kanuni za Idara ya Huduma za Binadamu Ilinois (IDHS) ambayo inasaidia kuhakikisha wataalamu wanaofanya kazi katika mfumo wa EI wa Illinois wana sifa stahiki na wanashiriki kila wakati katika maendeleo ya kitaalamu kuhusu medani yao ili kukuza uelewa wao wa watoto wenye uchelewaji wa kukua au ulemavu.

**IDHS**
Tafadhali tazama *Idara ya Huduma za Binadamu Illinois.*

**IEP**
Tafadhali tazama *Programu ya Elimu Binafsi.*

**IFSP**
Tafadhali tazama *Mpango Binafsi wa Huduma kwa Familia (IFSP).*

**Kikao cha Awali**
*Intake Meeting*
Baada ya *rufaa*, mchakato wa waratibu wa huduma kuwasiliana na familia na kupanga miadi ya kujadili Programu ya Afua za Awali, ikiwemo huduma na ada, haki za familia, na kufanya uchunguzi wa awali wa kitiba. Miadi ya awali inaipa familia fursa ya kumuuliza mratibu

wao wa huduma maswali na kushirikisha taarifa kuhusu mtoto wao na familia yao.

**Kipindi cha mpito**
*Transition*
Mchakato uliopangwa wa kusaidia watoto wenye au walio katika hatari ya uchelewaji wa kukua kuhama kati ya programu moja na nyingine, ikiwemo programu ya EI. Mifano ya mpito inajumuisha kutoka hospitali na kwenda nyumbani au kutoka katika huduma za EI na kwenda programu ya elimu ya awali. Timu ya IFSP inawajibika kuandaa mpango wa maandishi wa mpito unaoelezea hatua muhimu za kuondoka bila hitilafu yoyote kwenye programu ya EI.

**Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu**
*Federal Poverty Level (FPL)*
Kipimo kulingana na kipato cha familia kinachotumika kubaini mtu au familia ina ustahiki wa kusaidiwa kupitia programu za serikali kuu. Kwa kawaida FPL inabadilika kila mwaka.

**Matokeo**
*Outcomes*
Kauli za kile ambacho wanafamilia wanataka kukiona kikitokea kwa mtoto wao na familia yao kutokana na ushiriki wao katika afua za awali. Matokeo ya familia na mtoto yanaweza kuweka mkazo kwenye eneo lolote la ukuaji wa mtoto au maisha ya familia ambayo familia inahisi inahusiana na uwezo wake wa kuboresha ukuaji wa mtoto. Mara nyingi matokeo yanajumuisha muktadha wa maisha halisi.

**Matokeo ya familia**
*Family outcomes*
Tazama *matokeo*.

**Mazingira Halisi**
*Natural Environments*
Nyumba na mazingira ya jumuiya ambapo watoto na familia nyingine zisizo na ulemavu zinaweza kushiriki. Sehemu C ya Sheria ya Maboresho ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu (IDEIA) ya mwaka 2004 inaamuru watoto wachanga na wadogo wenye uchelewaji au ulemavu wahudumiwe katika mazingira halisi.

**Mbinu**
*Strategies*
Seti ya vitendo vinavyoweza kutekelezwa ili kumsaidia mtoto na familia yake kufikia matokeo tarajiwa. Mbinu kwa kawaida zinatokana na jinsi watoto wanavyojifunza katika maisha ya kila siku nyumbani, kwenye jumuiya, na katika mazingira ya ulezi na elimu ya awali.

**Mpango Binafsi wa Huduma kwa Familia**
*Individualized Family Service Plan (IFSP)*
Mpango ulioandikwa wa afua za awali unaoandaliwa na kutekelezwa na wazazi wa mtoto na timu ya afua za awali yenye wataalamu mbalimbali. IFSP inazingatia vipaumbele, wasiwasi, rasilimali, na malengo ya familia kwa ajili ya mtoto wao. Taarifa hii, sambamba na mawazo kutoka upimaji na tathmini za ziada, inawekwa rasmi katika mpango wa huduma na usaidizi kwa mtoto na familia katika mazingira yao halisi.

**Mpango wa Section 504**
*Section 504 Plan*
Mpango wa Section 504 unatoa ufikio wa maboresho na huduma husika kwa mtoto wako kutoka kwenye shule ya umma. Tofauti na IEP, mpango wa Section 504 haukomei tu kwa wanafunzi wenye ulemavu waina fulani.

**Mratibu wa Huduma**
*Service Coordinator*
Mwajiriwa wa ofisi ya CFC anayewajibika kwa shughuli za *uratibu wa huduma*, ikiwemo kuratibu huduma za EI na zisizo za EI kwa familia zilizoandikishwa kwenye programu ya EI.

**Msaidizi Maalum wa Wazazi**
*Parent Liaison*
Mzazi au mlezi wa mtoto mwenye uchelewaji au ulemavu na ambaye amepata idhini ya kuwa msaidizi maalum wa wazazi anaweza kutoa huduma za moja kwa moja za usaidizi kwa familia. Watu hawa wanaweza pia kutoa ushauri kwa wajumbe wa timu na watoa huduma wengine kuhusiana na mitazamo ya familia.

**Mtetezi**
*Advocate*
Mtu anayetetea au kuunga mkono mtu, jambo, au sera fulani. Watetezi wa familia wanawasaidia wazazi na wanafamilia wengine kutafuta na kuelewa huduma na chaguzi za afua za awali.

**Mtoa Huduma ya Afua za Awali**
*Early Intervention Provider*
Mtaalamu aliyeidhinishwa na/au aliyesajiliwa katika programu ya EI kutoa huduma kwa watoto wenye hatari ya *uchelewaji wa kukua*. Watoa huduma ya EI wanaidhinishwa na Idara ya Huduma za Binadamu Illinois (IDHS). Wanaweza kujumuisha wataalamu wa tiba vitendo, wataalamu wa tiba ya ukuaji, wataalamu wa tiba ya kimwili, na madaktari wa tiba ya matamshi-lugha.

**Nyanja**
*Domains*
Maeneo matano makuu ya ukuaji ambayo yanashughulikia akili, lugha, masuala ya kijamii na kihisia, stadi za kubadilika kulingana na mazingira, na stadi za kimwili, ikiwemo kusikia na kuona.

**Ofisi za Child and Family Connections (CFC)**
*Child and Family Connections (CFC) Offices*
Hizi ni ofisi 25 zinazofadhiliwa na Idara ya Huduma za Binadamu Illinois (IDHS) ambazo zinahudumia kama vituo muhimu vya kanda vya kuingia kwenye Programu ya Afua za Awali Illinois (EIP). Wajibu wa ofisi ya CFC unajumuisha shughuli za Child Find, ziara za familia, uratibu wa tathmini na ubainifu wa ustahiki kwa watoto, usimamizi wa uandaaji wa mipango binafsi ya huduma kwa familia (IFSP), na uratibu endelevu wa huduma, ikiwemo kubadilisha huduma baada ya mtoto kufikisha miaka 3.

**Programu ya Afua za Awali Illinois**
*Illinois Early Intervention Program*
Programu ya jimbo zima, ya kina, inayoratibiwa, inayohusisha mashirika mbalimbali ambayo yanazisaidia familia zenye watoto, wachanga hadi miaka 3, wenye hatari ya uchelewaji wa kukua, kupokea rasilimali na usaidizi ambao unawasaidia kuboresha ukuaji wa mtoto wao.

**Programu ya Elimu Binafsi (IEP)**
*Individualized Education Program*
Waraka unaopitiwa kila mwaka unaotakiwa na Sheria ya Maboresho ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (IDEIA) ya mwaka 2004 kwa watoto walio katika elimu maalum, wenye miaka 3 na kuendelea. IEP inaundwa na wazazi, walimu, watoa huduma, na wafanyakazi wa shule ambao wanabuni mpango wa mafundisho, ikiwemo malengo ya kila mwaka, mbinu za upimaji, na utoaji wa usaidizi na huduma za elimu maalum.

**Rasilimali**
*Resources*
Watu, mashirika, nyenzo, na usaidizi mwingine unaopatikana kwa familia ambao unaweza kutumika kusaidia uwezo wao wa kumtunza mtoto wao au kunufaika na huduma za EI kwa mtoto wao.

**Ridhaa Baada ya Kuarifiwa**
*Informed Consent*
Mchakato ambao familia zinathibitisha kwa maandishi kwamba (1) zimearifiwa kikamilifu kuhusu taarifa zote zinazohusiana na shughuli ya afua za awali, (2) zinakubali kutekeleza shughuli ambayo imeombewa ridhaa, na (3) zinaelewa ya kwamba utoaji wa ridhaa ni jambo la hiari kwao.

**Rufaa**
*Referral*
Kitendo chochote kinachowapeleka watoto na familia kwenye Ofisi mahalia ya CFC, inayowasaidia kufikia rasilimali na/au taarifa zilizopo. Yeyote anayeshuku mtoto ana uchelewaji au yupo katika hatari ya uchelewaji anaweza kutoa rufaa kwa kuwapigia Ofisi mahalia ya CFC.

**Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu**
*Individuals With Disabilities Education Act (IDEA)*
Sheria kuu iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1997 na mwaka 2004 ambayo ni marekebisho ya Sheria ya Elimu kwa Watoto Wote Vilema (EAHCA) ya mwaka 1975. IDEA inahakikisha huduma kwa watoto wenye ulemavu nchi nzima na inaongoza majimbo na mashirika ya umma kutoa huduma hizi. Sehemu B inaweka mkazo kwenye huduma kwa watoto wa elimu ya awali na wenye umri wa kwenda shule wenye ulemavu wa ukuaji. (Tazama pia *Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu [Sehemu C]*.)

**Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu (Sehemu C)**
*Individuals With Disabilities Education Act (IDEA) (Part C)*
Sehemu ya sheria kuu inayoweka mkazo kwenye huduma kwa watoto wachanga walio katika hatari ya uchelewaji wa kukua. (Tazama pia *Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu*.)

**Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia**
*Family Educational Rights and Privacy Act (FERPA)*
Sheria kuu inayolinda faragha ya rekodi za elimu za wanafunzi. Sheria hii inahusika kwa mashirika ya jimbo na mahalia ambayo yanayofadhiliwa na programu husika ya Idara ya Elimu ya Marekani.

**Sheria ya Uhamishaji na Uwajibikaji wa Bima ya Afya**
*Health Insurance Portability and Accountability Act (HIPAA)*
Sheria ya serikali kuu ambayo ilihitaji uundaji wa viwango vya kitaifa ili kulinda taarifa nyeti za afya za wagonjwa dhidi ya kufichuliwa bila ridhaa na uelewa wa mgonjwa.

**Tathmini/Upimaji**
*Assessments/Evaluations*
Zinaweza kuwa rasmi au si rasmi. Tathmini rasmi ya awali inabaini ustahiki wa huduma na inafanywa katika nyanja tano za ukuaji (tazama hapo chini) na timu yenye wataalamu mbalimbali. Tathmini rasmi za mara kwa mara pia hufanyika wakati mtoto yupo katika programu ya EI Illinois. Tathmini endelevu zisizo rasmi zinatumika kubaini uwezo na mahitaji ya mtoto mwenye ustahiki, pamoja na wasiwasi, vipaumbele, na rasilimali za familia zinazohusiana na mtoto.

**Uchelewaji wa Kukua**
*Developmental Delay*
Hali ya mtoto ambaye hajifunzi stadi mpya katika umri wa kawaida na/au anaonesha tabia isiyo sahihi kwa umri wake.

**Ulemavu**
*Disability*
Ulemavu wa kimwili na kiakili ambao unapunguza kwa kiasi kikubwa shughuli kubwa za maisha kama vile kusikia, kuona, kuzungumza, kutembea, kujijali, kusonga, kujifunza, au kufanya kazi.

**Umri wa Kukua**
*Developmental Age*
Unabainishwa kwa kupima umri ambao mtoto wako anaonesha stadi mbalimbali dhidi ya umri ambao stadi hizo zinachukuliwa kuwa jambo la kawaida. Umri wa kukua unabainishwa kupitia tathmini rasmi.

**Upatanishi**
*Mediation*
Chaguo moja katika programu ya EI Illinois ambalo wazazi wanaweza kuliomba wanapokuwa na lalamiko la mtoto kuhusiana na huduma na

wanataka kufikia mwafaka na upande mwingine. Upatanishi ni jambo la hiari na linalokubaliwa na pande zilizo katika mgogoro na unafanywa na mpatanishi mwadilifu mwenye sifa.

**Uratibu wa Huduma**
*Service Coordination*
Shughuli zinazofanywa na mratibu wa huduma ili kumwezesha mtoto mwenye ustahiki na familia yake kupokea huduma zilizoidhinishwa katika programu ya EI Illinois. Shughuli hizi zinaweza kujumuisha kupewa rufaa, na kuhakikisha ulindaji wa taratibu, kulinda haki, kuweka kumbukumbu ya huduma, kutoa taarifa kuhusu huduma, na kusaidia kubaini malengo.

**Usiri**
*Confidentiality*
Matarajio kwamba watoa huduma za EI watazuia ufikio wa taarifa kuhusu watoto na familia wanazozihudumia katika afua za awali. Programu ya EI inafuata miongozo na taratibu zote kulingana na Sheria ya Uhamishaji na Uwajibikaji wa Bima ya Afya (HIPAA) na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (FERPA) ili kuhakikisha haki na faragha na usiri wa familia.

**Vipaumbele**
*Priorities*
Mambo ambayo ni muhimu kwako na kwa familia yako kulingana na maadali na utamaduni wenu wa kipekee. Vipaumbele vinaweza kuisaidia timu ya IFSP kuandaa matokeo yenye tija kwako na kwa familia yako.

**Ziara za Video Mbashara**
*Live Video Visits (teletherapy)*
Huduma za EI zinatolewa kwa kutumia jukwaa la mtandaoni ili kuwasiliana na mzazi/mlezi na mtoto kupitia intaneti kwa kutumia video na sauti katika wakati halisi. Watoa huduma za EI wanaotoa huduma kwa njia hii wanatakiwa kupata mafunzo kuhusu ziara za video mbashara.

NYONGEZA C

# Fasili za Huduma za Afua za Awali

**Huduma za kisaikolojia/ushauri nasaha**
*Psychological/counseling services*
Huduma hizi zinasaidia kuboresha utendaji wa kisaikolojia wa mtoto na/au familia. Mifano inajumuisha upimaji wa kisaikolojia na ukuaji kwa mtoto, ushauri nasaha kwa familia, mafunzo ya wazazi na programu za elimu.

**Huduma za kitiba (kwa uchunguzi wa kitiba au tathmini tu)**
*Medical services (only for diagnostic or evaluation purposes)*
Huduma zitolewazo na daktari ili kusaidia uchunguzi au tathmini ya mtoto ili kubaini hali ya ukuaji wake na hitaji la huduma za afua za awali.

**Lishe**
*Nutrition*
Huduma za lishe zinaweza kujumuisha kushughulikia historia ya lishe ya mtoto na ulaji wa chakula, stadi za ulishaji na matatizo ya ulishaji, na tabia na mapendeleo ya chakula. Mifano inajumuisha kuandaa na kufuatilia mpango wa kushughulikia mahitaji ya lishe ya mtoto. Inaweza pia kujumuisha rufaa kwenye rasilimali za jumuiya.

**Lugha ya ishara au lugha ya mikono**
*Sign language or cued language*
Lugha ya ishara inaweza kujumuisha Lugha ya Ishara ya Amerika, ambayo ni lugha asilia inayotumia ishara za mikono. Matamshi mikono (cued speech) ni uwasilishaji wa kipicha wa lugha nyingine ila Lugha ya Ishara ya Amerika ni lugha inayojitegemea.

**Macho**
*Vision*
Mafunzo ya stadi za mawasiliano, mafunzo ya mjongeo, mafunzo ya uono, na mafunzo ya ziada kuunga mkono uwezo wa uono na misogeo. Mifano inajumuisha tiba ya macho na mafunzo ya uono.

**Matibabu ya audiolojia/usikiaji**
*Audiology/aural rehabilitation*
Huduma zinazosaidia kuzuia au kutibu tatizo la kusikia, kama vile mafunzo ya usikivu; matibabu ya usikiaji; vifaa vya kusoma na kusikiliza matamshi; vipimo vya kusikia na visaidizi vya kusikia kwa mtoto; mafunzo ya vifaa vya kusikia, na huduma nyingine kama hizo.

**Teknolojia saidizi**
*Assistive technology*
Kifaa chochote kinachosaidia uwezo wa mtoto kushiriki kivitendo nyumbani, programu ya ulezi wa watoto, au mazingira ya jumuiya. Neno hili halijumuishi kifaa cha kitiba kinachopandikizwa kwa upasuaji (k.m., cochlear implant) au uboreshaji (k.m., mapping), ukarabati, au ubadilishaji wa kifaa hicho. Mfano ni iPads, helmeti, kisaidizi cha kusimama, mipira ya mazoezi, ubao wa picha, kifaa cha kuonesha mahali kichwa kilipo, vikombe maalum, vijiko maalum, kompyuta, na vifaa vya mawasiliano kwa watu wasioweza kuzungumza (AAC).

**Tiba maungo**
*Physical therapy*
Mtaalamu wa tiba maungo anaweza kushughulikia maendeleo ya miendo ya mtoto. Stadi za miendo huwezesha watoto kufanya shughuli zinazohusisha misuli mikubwa (k.m. kutembea, kutambaa, kusimama, kupanda ngazi). Kwa watoto, hii inaweza kujumuisha kuwasaidia kujimudu kwa ajili ya ratiba za kila siku, kutumia vichezeo kulingana na mchezo husika, na kupanua chaguzi za usongaji.

**Tiba vitdo**
*Occupational therapy*
Wataalamu wa tiba vitendo wanaweka mkazo kwenye mambo tunayotaka na kuhitaji kufanya katika maisha yetu ya kila siku. Wataalamu wa tiba vitendo wanatumia shughuli za maisha ya kila siku (ratiba) kuendeleza afya, ustawi, na uwezo wetu wa kushiriki katika shughuli muhimu katika maisha yetu. Kwa watoto, mara nyingi hii inamaanisha kuunga mkono michezo na shughuli nyingine za maisha ya kila siku kama vile kula na kuvaa.

**Tiba ya Matamshi-lugha**
*Speech-language pathology*
Huduma za kuboresha mawasiliano na/au stadi za lugha. Mifano inajumuisha mtaalamu wa tiba ya matamshi-lugha anashirikiana na mtoto kusema maneno, utamkaji, kuunganisha maneno pamoja, na kutumia mawasiliano kwa watu wasioweza kuzungumza (AAC).

**Tiba ya ukuaji/mafunzo maalum**
*Developmental therapy/special instruction*
Mtaalamu wa tiba ya ukuaji atapima ukuaji wa jumla wa mtoto kwa kufanya tathmini katika maeneo matano: kiakili, kuwasiliana, kimwili, kijamii na kihisia, na kubadiika kulingana na mazingira. Tiba ya ukuaji inalenga maeneo haya matano ili kuongeza hali ya kujitegemea ya mtoto na kusaidia kufikia matokeo ya familia. Mifano inajumuisha kusaidia kutoa huduma katika mazingira ya mtoto, kupendekeza njia ambazo vitu vya kawaida vya nyumbani vinaweza kusaidia kufikia matokeo, na kuwa kama 'msiri' wa masuala yanayoitatiza familia.

**Ukalimani na utafsiri katika lugha nyingine**
*Interpretation and translation into other languages*
Huduma za ukalimani na utafsiri huzisaidia familia kuwasiliana na timu yao na kuhakikisha kwamba familia zina nyenzo katika lugha yao ya kwanza ili kusaidia kuelewa. Mifano inajumuisha mkalimani anayehudhuria kikao na kutafsiri nyaraka.

**Uratibu wa huduma**
*Service coordination*
Mchakato wa kivitendo na endelevu unaosaidia na kuwezesha familia kufikia huduma na unahakikisha haki za familia na ulindajii wa taratibu. Mifano inajumuisha kuratibu na kutekeleza upimaji na tathmini; kuwezesha na kusaidia kuandaa, kupitia, na kutathmini IFSP; kusaidia familia kubaini watoa huduma waliopo; kuratibu na kufuatilia utoaji wa huduma; kuzitaarifu familia kuhusu huduma za utetezi; kuratibu watoa huduma za kitiba na kiafya; na kuwezesha kuhamia kwenye huduma za elimu ya awali.

**Usafiri**
*Transportation*
Usafiri ambao unamwezesha mtoto kushiriki katika huduma za afua za awali. Mfano ni kuwafidia wazazi kwa usafirishaji wa watoto wao kwenda na kurudi katika huduma za afua za awali.

**Ushauri wa kiafya**
*Health consultation*
Ushauri wa kiafya ni ushauri kati ya tabibu mwenye leseni ambaye ametoa matibabu kwa mtoto katika mwaka uliopita na wajumbe wa timu ya IFSP ya mtoto kuhusiana na athari ya mahitaji ya kiafya ya mtoto kwenye utoaji wa huduma.

**Ustawi wa jamii**
*Social work*
Ustawi wa jamii unaweza kutoa usaidizi wa kihisia kwa familia. Mifano inajumuisha afisa wa ustawi wa jamii kubaini na kuratibu rasilimali za jumuiya, elimu kwa wazazi, ushauri nasaha, na kutatua matatizo.

**Uuguzi**
*Nursing*
Uuguzi unalenga kuzuia matatizo ya kiafya, kurejesha na kuboresha utendaji, na kuendeleza afya na ukuaji wa mtoto. Hii inaweza kujumuisha kutoa tiba na matibabu yaliyoainishwa na daktari wakati wa huduma za afua za awali za mtoto.

NYONGEZA D

# Sampuli ya Maelezo/Barua pepe kwa Ofisi za CFC

*Jumuisha jinsi gani na lini ungependa wajumbe wa timu ya EI wakujibu (k.m. wasiliana nami kwa barua pepe ___ au simu ____).*

## Kuomba Matokeo ya Tathmini

Mpendwa [SERVICE COORDINATOR],

Tunatumaini u mzima wa afya. Tunasubiri kwa hamu kikao cha mtoto wetu tarehe [DATE]. Kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za afua za awali, tunataka kuwa washirika sawa katika ufanyaji maamuzi ya mtoto wetu. Ili kufanya hivi, tunahitaji kuelimishwa na kutaarifiwa kikamilifu kuhusu maendeleo na mahitaji ya mtoto wetu.

Kwa lengo hili, tunaomba kuona rasimu ya [EVALUATION REPORTS] siku tatu za kazi kabla ya kikao husika. Tunaelewa kwamba wewe na wajumbe wa timu ya IFSP mna kazi nyingi. Tunatumaini kwamba tukizipitia nyenzo hizo kabla ya kikao, tunaweza kufanya kikao kilicho fanisi na wajumbe wote wa timu mnamo tarehe [DATE].

Asante kwa msaada wako katika ombi hili.

[NAME]

## Kuomba Badiliko la Mtoa Huduma

Mpendwa [SERVICE COORDINATOR],
Natumaini u mzima wa afya. Kama ujuavyo, mwanangu anahudumiwa na [NAME] kama [TYPE OF PROVIDER] wake. Amekuwa akionwa na [NAME] kwa miezi [XX] iliyopita. Kwa bahati mbaya, mtoa huduma huyu si sahihi kwa familia yetu. Hatujaona aina ya maendeleo tuliyotarajia na tunahisi mtoa huduma mpya anaweza kufanya kazi nzuri zaidi. Hivyo basi, naomba mtoa huduma mpya.

Nasubiri kwa hamu kuongea nawe kuhusu hili na kupata mtoa huduma atakayetufaa zaidi.

Asante, [NAME]

## Kuomba Mratibu Mpya wa Huduma

Mpendwa [CFC MANAGER],

Natumaini u mzima wa afya. Kama ujuavyo, familia yetu inahudumiwa na [NAME] kama mtoa huduma wetu. [NAME] amefanya kazi nasi kwa miezi [XX] iliyopita. Kwa bahati mbaya, hatuoni kama ni mtu sahihi kwa familia yetu. Hivyo, naomba mratibu mpya wa huduma kwa [CHILD'S NAME].

Nasubiri kwa hamu kuongea nawe kuhusu hili na kupata mratibu wa huduma atakayetufaa zaidi.

Asante,

[NAME/JINA]

## Kuomba Badiliko la Huduma

Mpendwa [SERVICE COORDINATOR],

Natumaini u mzima wa afya. Naandika kuhusu mtoto wangu, [NAME]. Kama ujuavyo, [NAME] amekuwa akipewa dakika [XX] za tiba ya matamshi kwa wiki kwa miezi [XX] iliyopita. Kama ilivyoainishwa katika maelezo ya maendeleo yake, hapigi hatua. Hapa nyumbani, sijaona badiliko au hatua yoyote kuelekea matokeo ya IFSP yake. Ningependa kuomba kikao cha timu ya IFSP ili kujadili badiliko kwenye huduma zetu za sasa.

Napatikana tarehe zifuatazo kwa ajili ya kikao cha IFSP ili kujadili jambo hili pamoja na timu:

- [DATE]
- [DATE]
- [DATE]
- [DATE]

Nasubiri kwa hamu kujadili wasiwasi wangu pamoja na timu na kutafuta njia nyingine itakayomwezesha [CHILD] kupiga hatua zenye tija zaidi.

Asante, [JINA]

# Sampuli ya Maelezo/Barua pepe kwa Ofisi za CFC (kwa Kiigereza)

*Hapo chini ni matoleo ya Kiingereza ya sampuli ya maelezo/barua pepe zinazoweza kutumwa kwa ofisi za CFC.*

## Kuomba Matokeo ya Tathmini

Dear [SERVICE COORDINATOR],

We hope you are doing well. We are looking forward to our child's meeting on [DATE]. As noted by the principles of early intervention, we want to be equal partners in decision-making for our child. To do this, we need to be educated and fully informed about our child's progress and needs.

To this end, we are requesting to see the draft of the [EVALUATION REPORTS] three business days before the meeting. We understand that you and the IFSP team members are busy. We hope that by reviewing the materials before the meeting, we can hold an efficient meeting with all team members on [DATE].

Thanks for your help with this request.

[NAME]

## Kuomba Badiliko la Mtoa Huduma

Dear [SERVICE COORDINATOR],

I hope you are doing well. As you know, my son has [NAME] as his [TYPE OF PROVIDER]. He has been seeing [NAME] for the past [XX] months. Unfortunately, this provider is not a good fit for our family. We haven't seen the kind of progress we were expecting and feel a new provider may work better. Thus, I am requesting a new provider.

I look forward to talking with you about this and finding a provider who is a better match.

Thank you, [NAME]

## Kuomba Mratibu Mpya wa Huduma

Dear [CFC MANAGER],

I hope you are doing well. As you know, our family has [NAME] as our service coordinator. [NAME] has been working with us for the past [XX] months. Unfortunately, it does not seem that this is a good fit for our family. Thus, I am requesting a new service coordinator for [CHILD'S NAME].

I look forward to talking with you about this and finding a service coordinator who is a better match for our family.

Thanks for your help with this request.

[NAME]

## Kuomba Badiliko la Huduma

Dear [SERVICE COORDINATOR],

I hope you are doing well. I am writing about my child, [NAME]. As you know, [NAME] has been receiving [XX] minutes of speech therapy per week for the past [XX] months. As noted on his progress notes, he is not making progress. At home, I have not seen any change or movement toward his IFSP outcomes. I would like to request an IFSP team meeting to discuss a change to our current services.

I am available on the following dates for an IFSP meeting to discuss this with the team:

- [DATE]
- [DATE]
- [DATE]
- [DATE]

I look forward to discussing my concerns with the team and finding a way to move forward that enables [CHILD] to make meaningful progress.

Thank you, [NAME]

NYONGEZA E

# Rasilimali kwa Familia Zilizopo Katika Afua za Awali

## Wabia wa EI Illinois

**Ofisi Kuu ya Kutoza Bili za Afua za Awali (EI-CBO)**
EI-CBO inashughulikia madai ya programu ya EI Illinois. EI-CBO inaidhinisha malipo, inashughulikia madai ya EI ya kila mwezi ya Medicaid, na inatoa data ili kuzisaidia CFC kukamilisha uthibitishaji wa awali wa mafao ya bima kwa familia. EI-CBO pia inadumisha mfumo wa ada ya ushiriki wa familia, inasimamia mchakato wa ukusanyaji mapato, na kutoa usaidizi wa kiufundi kwa familia na watoa huduma za EI. Pia inasimamia huduma ya bure ambayo inatoza kampuni za bima kwa niaba ya watoa huduma za EI. Fahamu zaidi kupitia https://eicbo.info

**Maktaba ya Afua za Awali (EIC)**
Maktaba ya Afua za Awali Illinois (EIC) ni kituo cha jimbo zima kwa familia na wataalamu wanaohudumia watoto wadogo. EIC inaweza kutoa taarifa kupitia machapisho na kwa njia za kidijitali kuhusu uzazi, ukuaji wa mtoto, elimu ya awali ya mtoto, elimu maalum, afua za awali, ulemavu na kasoro mahsusi, uchelewaji wa kukua, na mada nyingine.  Taarifa zinaweza kutolewa kwa miundo mbalimbali (chapisho, dijitali) na lugha mbalimbali. Pia EIC inaazimisha iPad na huduma ya intaneti kwa familia ili ziweze kushiriki katika afua za awali kupitia ziara za video mubashara. Fahamu zaidi kupitia https://eiclearinghouse.org/

**Programu ya Kufuatilia Afua za Awali (EIMP)**
Dhumuni la programu hii ni kuhakikisha kwamba kanuni za jimbo na serikali kuu kuhusiana na utoaji wa huduma za EI Illinois zinazingatiwa kwa kutoa ushahidi wa nyaraka, kuchunguza malalamiko, kufanya mapitio ya watoa huduma na CFC, na kuhakikisha uzingatiaji wa sera. Fahamu zaidi kupitia https://www.earlyinterventionmonitoring.org/

**Programu ya Mafunzo ya Afua za Awali (EITP)**
EITP inatoa huduma ya ukuaji wa kitaalamu, saa za leseni/mkopo, na usaidizi wa kiufundi kwa wafanyakazi wa CFC, watoa huduma za EI, na wadau wengine. Tovuti yake inajumuisha taarifa kuhusu jitihada za ushirikiano kati ya mifumo mbalimbali na data ya mfumo wa afua za awali. Fahamu zaidi kupitia https://eitp.education.illinois.edu/

**Chama cha Watoa Huduma (PC)**
Chama cha Watoa Huduma ni ofisi ya kuidhinisha na kuandikisha watoa huduma wa afua za awali wanaofanya kazi Illinois. Tovuti yake inajumuisha habari muhimu zinazowalenga moja kwa moja watoa huduma za EI na ni eneo kuu la sera, taratibu, na habari za malipo za IDHS. Fahamu zaidi kupitia https://providerconnections.org/

## Rasilimali Nyingine za Jimboni

**Marekebisho ya Mazingira ya Ulezi kwa Watoto Wenye Ulemavu (ACSCWD)**
Rasilimali hii inatoa marekebisho yenye haki kisheria kwa ajili ya mtoto wako katika mazingira ya ulezi wa watoto. Fahamu zaidi kupitia https://www.ada.gov/topics/child-care-centers/

**Tao la Illinois (Arc of Illinois)**
Tao (The Arc) inatoa rasilimali na taarifa, inazisaidia familia katika jitihada zao binafsi za utetezi, na inatoa mafunzo na kuelimisha watu wenye ulemavu, familia, na wataalamu. Pia inatoa ufadhili wa teknolojia na fidia kwa familia ili kuhudhuria mikutano inayohusiana na masuala ya ulemavu. Fahamu zaidi kupitia https://www.thearcofil.org/

**Rasilimali na Rufaa za Ulezi wa Watoto (CCR&R)**
Ofisi yako mahalia ya CCR&R inaweza kukusaidia

kupata watoa huduma za ulezi wa watoto walio karibu nawe na kuona iwapo una ustahiki wa kusaidiwa kulipia huduma ya ulezi wa watoto. Fahamu zaidi kupitia https://www.inccrra.org/about/sdasearch

**Divisheni ya Matibabu Maalum kwa Watoto (DSCC)**
Divisheni ya Matibabu Maalum kwa Watoto inaweza kuzisaidia familia zenye ustahiki kufikia huduma za afya na usaidizi wa kifedha kwa watoto wadogo wenye matatizo fulani sugu. "Core Program" inahudumia idadi kubwa sana ya watoto wenye mahitaji maalum ya huduma za afya na inatoa bure uratibu wa tiba. "Home Care Program" inatoa uratibu wa tiba kwa watoto wenye matatizo mengi ya kitiba ambao ni dhaifu kiafya na tegemezi kwa teknolojia au uuguzi wa zamu nyumbani. Fahamu zaidi kupitia https://dscc.uic.edu/

**Kituo cha Usaidizi wa Kiufundi cha Afua za Awali (ECTAC)**
Kinakupa data na taarifa zinazohusiana na watoto wachanga, ikiwemo afua za awali. Fahamu zaidi kupitia https://ectacenter.org/

**Ziara za Nyumbani**
Wanaozuru nyumbani kazi yao ni kuboresha stadi za uzazi nyumbani. Ilinois ina programu kadhaa za kuzuri nyumbani. Kuona kama kuna programu ya kuzuri nyumbani karibu nawe, tembelea https://igrowillinois.org/find-a-program/

**Mradi wa Teknolojia Saidizi Illinois (IATP)**
Mradi wa Teknolojia Saidizi Illinois unafanya tathmini za teknolojia saidizi, unaazimisha vifaa (bure) kwa familia, na kuzisaidia familia kupata njia za kulipia vifaa husika. Fahamu zaidi kupitia https://iltech.org/

**Kituo cha Watoto Illinois (ICK)**
Kituo cha Watoto Illinois ni kituo ambapo wazazi, wazakuu, walezi, walimu, na watoa huduma ya ulezi wa watoto wa Illinois wanaweza kufikia vitu vyote vinavyohusiana na watoto katika jimbo la Illinois. Kituo hiki kinafadhiliwa na IDHS na kusimamiwa na INCCRRA. Fahamu zaidi kupitia https://www.illinoiscaresforkids.org/

**Mradi wa Ujifunzaji wa Awali Illinois (IEL)**
Unatoa taarifa zenye ushahidi za watoto wadogo katika jimbo la Illinois. Fahamu zaidi kupitia https://illinoisearlylearning.org/

**Programu ya Msamaha wa Huduma za Nyumbani na Jumuiya**
Programu ya HCSWP inatoa huduma zinazowawezesha watu kubaki nyumbani kwao au kuishi katika mazingira ya jumuiya badala ya taasisi. Programu hii ya msamaha inatoa ufadhili kwa mtoto wako kuendelea kuishi nyumbani na wewe pamoja na usaidizi unaohitajika. Fahamu zaidi kupitia https://hfs.illinois.gov/medicalclients/hcbs.html

**Muungano wa Faraja (Illinois Respite Coalition)**
Kama mzazi wa mtoto mwenye ulemavu au uchelewaji, unaweza kuwa na usathiki wa kupokea ulezi wa mtoto bure nyumbani kwako. Fahamu zaidi kupitia http://www.illinoisrespitecoalition.org/

**Vituo vya Mafunzo na Taarifa kwa Wazazi (PTI)**
PTI ni vituo vinavyofadhiliwa na serikali kuu vilivyokusudiwa kuelimisha na kuwawezesha wazazi kuhusu haki zao za elimu maalum (kwa watoto wenye ulemavu na/au uchelewaji kuanzia uchanga hadi miaka 26). Vituo vya PTI vinatoa mafunzo ya bure, rasilimali, rufaa, na usaidizi binafsi. Kuna vituo viwili vya PTI katika jimbo la Illinois.

- Family Resource Center on Disabilities (FRCD) kinahudumia familia zilizopo wilaya za McHenry, Lake, Kane, DuPage, Cook, Will, Kendall, na Grundy (www.frcd.org)
- Family Matters kinahudumia wilaya nyingine zote katika jimbo (https://www.fmptic.org/)

**Shirika la Ulindaji na Utetezi (PAA)**
Shirika linalofadhiliwa na serikali kuu ambalo linatoa usaidizi wa kisheria bure kwa familia na watu wa umri wote wenye ulemavu. Fahamu zaidi kupitia https://www.equipforequality.org/

NYONGEZA F

# Matokeo: Kupima Mafanikio ya EI



## Wyniki rodziny

W ramach uczestnictwa we wczesnej interwencji pomożemy ci zdobyć wiedzę i umiejętności w tych trzech kluczowych obszarach:

- Kujua haki zako
- Kushirikisha mahitaji ya mtoto wako
- Kuchukua hatua sahihi ili kukidhi mahitaji ya mtoto wako

## Matokeo ya Mtoto

Ni muhimu kujua jinsi mtoto wako anavyokua kama matokeo ya kupewa huduma za afua za awali. Unamuona mtoto wako katika shughuli na mazingira ambayo wajumbe wengine wa timu hawamuoni. Matokeo matatu ya mtoto ni:

- Kujenga mahusiano chanya ya kijamii
- Kupata na kutumia maarifa na stadi
- Kuchukua hatua sahihi ili kukidhi mahitaji yake

## Matokeo Fanisi ya IFSP

Matokeo fanisi ni manufaa au matunda unayotaka kwa mtoto wako na familia yako kama matokeo ya kushiriki katika afua za awali. Matokeo haya yanatija katika maisha yako ya kila siku na yanawekwa katika mpango binafsi wa huduma kwa familia (IFSP) ambao uliuandaa pamoja na timu yako ya EI.

## Una Jukumu Muhimu Katika Ukuaji wa Mtoto Wako

Kama mjumbe wa timu ya EI, ushiriki wako wa kivitendo ni muhimu kwa sababu wewe ndiye unayemjua vizuri zaidi mtoto wako. Unawezaje kusaidia?

- Mchunguze mtoto wako ukiwa nyumbani na maeneo ya jumuiya
- Shirikisha unachokijua kwa wajumbe wengine wa timu ya EI
- Uliza timu yako ya EI ikiwa una maswali kuhusu mtoto wako
- Jibu Maswali ya Utafiti wa Matokeo ya Familia

Kufahamu zaidi kuhusu matokeo ya mtoto na familia, tembelea https://eiclearinghouse.org/blogs/outcomes-types/

NYONGEZA G

# Maelezo ya Kikao Chetu cha IFSP

**Nilihudhuria kikao chetu cha IFSP tarehe** ____________________

**Wengine waliohudhuria:**

| Majina | Jukumu kwenye Timu |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

**Mambo muhimu niliyojua kuhusu mtoto wangu katika kikao cha IFSP:** ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

**Matokeo muhimu tuliyobaini kwa ajili ya familia na mtoto wangu:** ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

NYONGEZA H

# Kanuni na Taratibu za Mazingira Halisi

1. Watoto wadogo wanajifunza vizuri zaidi kupitia uzoefu na miingiliano ya kila siku na watu waliowazoea katika mazingira waliyoyazoea.

2. Familia zote, kupitia usaidizi na rasilimali muhimu, zinaweza kuboresha ujifunzaji na ukuaji wa watoto wao.

3. Jukumu kuu la mtoa huduma wa afua za awali ni kushirikiana na kuwasaidia wanafamilia na walezi katika maisha ya watoto.

4. Mchakato wa afua za awali, kuanzia mwanzo hadi kuhama huduma, unapaswa kuwa madhubuti na wa binafsi ili kuakisi mapendeleo, mitindo ya kujifunza, na imani za kitamaduni za mtoto na wanafamilia.

5. Matokeo ya IFSP lazima yawe fanisi na yanayotokana na mahitaji ya watoto na familia na vipaumbele vilivyobainishwa na familia.

6. Vipaumbele, mahitaji, na maslahi ya familia yanashughulikiwa vizuri zaidi na mtoa huduma mkuu anayewakilisha na kupewa usaidizi wa timu na wa jumuiya.

7. Afua kwa watoto wadogo na wanafamilia lazima zitokane na kanuni zilizo wazi, taratibu zilizothibitishwa, utafiti bora uliopo, na sheria na kanuni husika.

**Chanzo:** Kikundi-kazi cha Kanuni na Taratibu katika Mazingira Halisi (Machi 2008).

*Dhima na Kanuni Kuu za Kutoa Huduma za Afua za Awali katika Mazingira Halisi*

NYONGEZA I

# Mfano wa Maelezo ya Maendeleo katika EI

**(Muhtasari wa Ziara, Kumbukumbu za Kila Siku)**

**Mtoa huduma:** Sara Smith
**Mtoto:** Ryan Jones

**Mlezi/Walezi:** Mary Jones
**EI #:** 123123

| Tarehe | Muhtasari | Muda wa Kuanza | Eneo |
|---|---|---|---|
| 3-17-21 | 60 | 8:30 am | Nyumbani |

**Ripoti ya mlezi:** Mary alieleza kwamba Ryan amezidisha suala la kutoa sauti na amekuwa akiketi zaidi peke yake. Alieleza kwamba anaweka uzito zaidi miguuni mwake wakati anapotembea. Anasema kwa kawaida huwa anachoka kufikia muda huu wa siku. Kuna siku, Mary na Ryan walikuwa wakipuliza mapovu (bubbles) na alijaribu kusema "povu."

**Leo tumefanyia kazi matokeo yafuatayo na mtoto wako**

- **Vitabu:** Ryan alijtahidi kufungua kurasa za vitabu. Baada ya rafiki zake kutoka nje, nilijaribu kumfanya abadilishe kitendo kutoka kuwa amelala na kuwa ameketi. Aliweka juhudi kidogo za kunisadia, hata baada ya mimi kumwomba na kusema "nisaidie." Hatimaye aliinuka na kunisaidia kufungua kurasa zaidi.
- **Kutambaa:** Alitambaa kuanzia zulia la kando ya kochi hadi zulia la kando ya bloku. Alijitahidi sana kuinuka kwa kutumia mikono na magoti yake. Pia alijitahidi sana kubabilisha kitendo kutoka kutambaa hadi kuketi lakini alionekana kufanya hivyo kwa kutumia upande wa kushoto. Alitambaa mara kadhaa, na haikuwa mpaka mwisho ndipo aliporudi katika mtindo wake wa kutambaa kijeshi.
- **Kutembea:** Alijitahidi sana nilipoweka mikono yangu makwapani mwake, hivyo nikaihamishia juu ya mikono wake. Hadi wakati tunapofika kwenye zulia kando ya kochi nilikuwa nimeshika vidole/viganja vyake tu. Nilikuwa nikitoa usaidizi mwingi sana, lakini kidogo sana kwa kutumia mikono yangu chini ya makwapa yake.
- **Kuiga sauti:** Leo aliiga baadhi ya sauti lakini alionekana kupendelea kutoa zaidi sauti zake mwenyewe kuliko kuiga. Tulipokuwa tukisoma, nilimwambia napaswa kujaribu kusoma kabla ya kufunua ukurasa, na kwa kawaida huwa anajaribu angalau kuniiga kwa sekunde kadhaa.

**Uchunguzi wa jumla:** Ryan ANAJITAHIDI sana katika kutambaa! Kuna wakati alipumzika na kulalia viwiko vyake ili aweze kupiga makofi yeye mwenyewe (HATUA KUBWA SANA)! Nilishangazwa si tu kwa jinsi alivyofanya vizuri lakini pia muda aliotumia kufanya hivyo. Leo aliweza kutambaa yeye mwenyewe na kuketi akitokea katika hali ya kujilalia. Alijitahidi sana pia alipopewa chaguzi kati ya "zaidi" na "mwisho" katika shughuli zote tulizofanya.

**Mambo ya kufanyia kazi kati ya ziara moja na nyingine:** Endelea kumhimiza Ryan kutambaa kwa mikono na magoti. Unaweza kujaribu kumtekenya magoti ikiwa haketi wima. Aliketi mara kadhaa nilipomtekenya magoti yake.

**Mpango wa ziara inayofuata:** Endelea kufanyia kazi kutambaa na kutembea katika ratiba za kawaida.

**Maswali ya walezi kuhusu miadi ijayo**
Mary aliuliza kiasi gani cha taarifa anapaswa kutoa kuhusu ziara hizi kwa mama na dada yake, ambao wakati mwingine wanamlea Ryan.

**Ziara ijayo**
Machi 31, 2024, 8:30 a.m.

IDHS
ILLINOIS DEPARTMENT
OF HUMAN SERVICES

Bureau of Early Intervention
823 E. Monroe St. • Springfield, Illinois 62701
https://www.dhs.state.il.us/page.aspx?item=30321